

Maria Valtorta

JAMBO!!! / HELLO!!!

RANGI MBICHI / WET PAINT !!!

ORIYO : HAIFANGI KAZI / ATTENTION : SITE UNDER CONSTRUCTION

Injili kama nilivyofunuliwa

KUZALIWA NA KUTAWA
KWA MARIA NAYESU
Sura 1- 43

MWAKA WA KWANZA WA MAISIIA
YA BWANAYESU WAZI KWAWATU
Sura 44 - 140

MWAKA WA PILI WA MAISIIA
YA BWANA YESU WAZI KWA WATU
Sura 141 - 312

MWAKA WA TATU WA MAISHA
YA BWANA YESU WAZI KWA WATU
Sura 313 - 540

MATAYARISHO
YA MATEO YA BWANA YESU
Sura 541 - 586

MATEO NA KIFO CHA BWANA YESU
Sura 587 - 613

UTUKUFU
WA BWANA YESU NA MARIA
Sura 614 - 649

CENTRO EDITORIALE VALTORTIANO

Maria Valtorta

Injili kama nilivyofunuliwa

KITABU CHA KWANZA

Sura 1 - 78

Kichwa cha asili
L'Evangelo come mi è stato rivelato
Volume Primo, Capitoli 1 - 78
Kimefasiriwa kutoka kiitaliani na
Gianluigi Martini kwa msaada wa
Sista Bernardina Allenspach

Kimetengenezwa na

ISBN 88-7987-017-3

Kimetengenezwa na

Centro Editoriale Valtortiano srl.

Kimechapishwa na

Tipografia Editrice M. Pisani sas. Isola del Liri

Printed in Italy, 1995

Sura zilizomo katika

Kitabu cha kwanza

Maisha ya mwandishi kwa kifupi

IX

Injili nne zilizounganishwa

XIV

KUZMNA NA KUTAWA KWA MARIA NAYESU

1	Fikira ya utangulizi.	2
	Mungu alitaka uzazi usio na doa.	
2.	Yoakine na Ana wanamwekea Mungu nadhiri moja.	3
3.	Sikukuu ya Vibanda.	7
	Yoakine na Ana walikuwa na Hekima	
4.	Ana anatangaza umama wake kwa zaburi.	11
	Mwilini mwake ni moyo wa Maria usio na dhambi.	
5.	Kuzaliwa kwa Maria.	16
	Ubikira wake katika fikira ya milele ya Baba.	
6.	Kutakasika kwa Ana na sadaka ya Maria,	30
	aliye Msichana mkamilifu kwa ufalme wa Mbinguni.	
7.	Maria mtoto pamoja na Ana na Yoakine.	34
	Hekima ya Mwana ni tayari midomoni mwake Maria.	
8.	Maria amepokewa Hekaluni. Yeye, katika unyenyekevu wake,	40
	hakujua ndiye ya kuwa amejaa Hekima.	
9.	Kufa kwa Yoakine na Ana kulikuwa kutamu, baada ya maisha	46
	ya uaminifu mwenye hekima kwa Mungu katika majaribu.	
10.	Wimbo wa Maria, akikumbuka	49
	mambo aliyoyaona rohoni kutoka kwa Mungu.	

11.	Maria amwamini Kuhani Mkuu nadhiri yake.	56
12.	Yosefu amechaguliwa kuwa bwana arusi wa Bikira.	59
13.	Arusi ya Bikira na Yosefu, aliyefundishwa na Hekima kuwa mlinzi wa Fumbo	64
14.	Wanaarusi wafika Nazareti.	71
15.	Mwisho wa Habari Njema ya kutangulia. V	77
16.	Kumpasha habari Maria.	78
17.	Kutotii kwa Hawa na kutii kwa Maria.	81
18.	Maria ampasha Yosefu habari kwamba Elisabeti amepata mimba na kumwamini Mungu shughuli ya kueleza hali yake mwenyewe.	90
19.	Maria na Yosefu waelekea Yerusalemu.	95
20.	Kuondoka katika Yerusalemu. Wajihi wa heri wa Maria. Umuhimu wa kusali kwa Maria na Yosefu.	96
21.	Kufika kwa Maria Hebroni na kukutana na Elisabeti.	100
22.	Kukaa katika Hebroni. Matokeo ya upendo wa Maria kwa Elisabeti.	104
23.	Kuzaliwa kwa Yohane Mbatizaji. Kila uchungu hutulia kifuani pa Maria.	111
24.	Kutahiri kwa Yohane Mbatizaji. Maria ni Chemchemi ya Neema kwa yule anayepokea Mwanga.	117
25.	Kutolewa kwa Yohane Mbatizaji Hekaluni na kuondoka kwa Maria. Mateso ya Yosefu.	121
26.	Yosefu amwombea Maria radhi. Imani, ukarimu na unyenyekevu kwa kumpokea Mungu.	127
27.	Tangazo la kujiandikisha. Mafundisho juu ya upendo kwa bwana arusi na juu ya kumtumaini Mungu.	131
28.	Kufika Betlehemu.	136
29.	Kuzaliwa kwa Yesu. Nguvu ya ukombozi ya umama wa kimungu wa Maria. j	140
30.	Kutangazwa kwa wachungaji, walio wa kwanza kumwabudu Neno aliyefanyika Mwanadamu.	147

31.	Kukaribisha kwa Zakaria. Utakatifu wa Yosefu na kuwatii makuhani.	156
32.	Kumtolea Bwana Yesu kwa Mungu Baba Hekaluni. Njema ya Simeoni na unabii wa Ana.	161
33.	Utumbuizo wa Bikira.	166
34.	Kuabudu kwa Mamajusi. Ni 'habari njema ya imani'.	169
35.	Kukimbilia Misri. Mafundisho kuhusu ono la mwisho kulingana na mji wa Bwana Yesu.	180
36.	Familia Takatifu huko Misri. Fundisho kwa familia zote.	188
VI		
37.	Somo la kwanza la kazi ya Yesu, asiyeipinga kanuni ya umri wake.	194
38.	Maria mwalimu wa Yesu, Yuda na Yakobo. 1	198
39.	Matayarisho kwa uzima wa Yesu na kuondoka katika Nazareti.	204
40.	Mtihani wa Yesu, aliyefika umri wa miaka kumi na miwili, Hekaluni.	208
41.	Mabishano Hekaluni kati ya Yesu na waalimu. Dhiki ya Mama Maria na jibu la Mwana.	212
42.	Kufa kwa Yosefu. Bwana Yesu yu amani ya wateswao na wafao.	221
43.	Mwisho wa maisha ya kufichwa.	228
MWAKA WA KWANMWAMAISIIAYABWANAYESUWAZI KWAWA'TU		
44.	Kuagana na Mama na kuondoka katika Nazareti. Kulia na kusali kwa Msaidizi wa Mwokozi.	231
45.	Kuhubiri kwa Yohane Mbatizaji na kubatizwa kwa Bwana Yesu . Matokeo ya kimungu.	238
46.	Bwana Yesu ajaribiwa na Iblisi nyikani. Jinsi ya kushinda katika vishawishi.	243
47.	Kukutana na Yohane na Yakobo. Yohane wa Zebedayo mwenye moyo safi katika wafuasi.	249

48.	Yohane na Yakobo wamsimulia Petro habari za mkutano wao na Masiha.	253
49.	Mkutano na Petro na Andrea baada ya hotuba katika sinagogi. Yohane wa Zebedayo ni mkuu hata katika unyenyekevu.	257
50.	Bwana Yesu kule Bethsaida nyumbani mwa Petro. Filipino na Nathanaeli wakutana na Yesu.	265
51.	Maria amtuma Yuda Thadayo amwite Bwana Yesu aje arusini huko Kana.	273
52.	Arusi kule Kana. Mwana, asipokuwa tena chini ya Mama,	277
53.	Bwana Yesu awafukuza wafanya biashara Hekaluni.	283
54.	Kukutana na Yuda wa Keriothi na Tomaso. Simoni Zelote ameponywa ukoma.	287
VII		
55.	Tomaso anawekewa jambo.	293
56.	Simoni Zelote na Yuda Thadayo wameungwa katika bahati moja.	298
57.	Bwana Yesu huko Nazareti pamoja na Yuda Thadayo na wanafunzi wengine sita.	304
58.	Kuponywa kwa kipofu huko Kafarnaumu.	308
59.	Mwenye pepo aponywa katika sinagogi ya Kafarnaumu.	313
60.	Bwana Yesu amponya mkwewe Simoni Petro.	319
61.	Bwana Yesu awafadhili maskini akisha sema mfano wa farasi aliyependwa na mfalme.	324
62.	Bwana Yesu anatafutwa na wanafunzi anaposali usiku.	330
63.	Mwenye ukoma ameponywa karibu na Korazini.	333
64.	Mwenye kupooza ameponywa huko Kafarnaumu.	337
65.	Mwujiza wa kupata samaki wengi, na uchaguzi wa mitume minne wa kwanza.	343
66.	Yuda Iskariote amefanyika mwanafunzi kwenye Gethsemane.	345
67.	Mwujiza wa mabapa ya visu yaliyovunjika,	348

68.	Bwana Yesu, Hekaluni pamoja na Iskariote, anafundisha.	352
69.	Bwana Yesu anamfundisha Yuda Iskariote.	358
70.	Bwana Yesu huko Gethsemani pamoja na Yohane wa Zebedayo. Mlingano wa Mwanafunzi mpendwa na Yuda.	363
71.	Kumjulisha Yuda Iskariote kwa Yohane na Simoni Zelote.	370
72.	Kwenda Betlehemu pamoja na Yohane, Simoni Zelote na Yuda Iskariote.	373
73.	Kule Betlehemu, nyumbani mwa mtu wa shamba na pangoni mwa kuzaliwa kwake Bwana Yesu.	376
74.	Bwana Yesu kule Betlehemu katika nyumba ya wageni na juu ya mabaki ya nyumba ya Ana.	386
75.	Bwana Yesu anakwenda kutazama wachungaji Eliya na Lawi.	396
76.	Kule Yuta kwa mchungaji Isaka. Sara na watoto wake.	402
77.	Bwana Yesu huko Hebroni nyumbani kwa Zakaria. Mkutano na Haglae.	410
78.	Kule Keriothi. Kifo cha mzee Sauli.	417
	Maelezo ya maneno yasiyojulikana sana	428
VIII		

Maisha ya mwandishi kwa Kifupi

Jamaa yake, masomo na malezi

Maria Valtorta, mwandishi wa kitabu hicho, alikuwa na roho isiyo ya kawaida. Kwa hiyo tunaandika maisha yake kutokana na maandiko yake na ya watu waliomfahamu vizuri.

Alizaliwa 14 Machi 1897 huko Kazerta katika nchi Italia kusini.

Alikuwa binti wa pekee wa wazazi wake: Baba Yosefu, mwema sana, alikuwa mwalimu wa lugha ya Kifaransa. Yeye aknaa mgumu na mkali.

Kwa sababu ya kazi ya baba yake mpendwa jamaa ya mwandishi ililazimishwa kuhama mji hata mji mara nyingi.

Mara ya kwanza Maria alipokuwa na mwaka mmoja na nusu wakaenda Faenza na baadaye katika mwaka 1901 Milano. Pale katika shule iliyoongozwa na masista, msichana huyu, kabla hajawa na umri wa miaka mitano, kwa mara ya kwanza alikutana na Mungu. Tangu hapo mtoto alifanya "bidii kubwa sana amtulize Yesu na kumwiga kwa mateso aliyochagua mwenyewe kwa mapendo'.

Oktober 1904 alikwenda shuleni kwa masista wa Marzellinus pale Milano. Baada ya muda mfupi alikuwa mtoto wa kwanza “kwa sababu ya akili yake na mapaji ya kiroho”. Pia pale alipata sakramenti ya Kipa Imara akiwa na umri wa miaka minane. Alipewa na Baba Kardinali Andrea Ferrari “ambaye kwa yeye Roho Mtakatifu wa Upendo humiminwa kweli”.

Tangu Septemba 1907 Maria alijifunza katika shule ya serikali pale Voghera pamoja na kupata masomo ya Kifaransa kwa masista waliokuwa wamefukuzwa kutoka Ufaransa.

Kwa ajili ya masista Maria aliweza kupokea sakramenti ya Komunyo ya kwanza katika mwezi wa Oktoba 1908. Maria alikuwa na uchungu kwa sababu baba yake hakuja kwa sikukuu yake ya Komunyo ya kwanza kwa sababu mama alifikiri "si lazima aje".

Ikiwa mama alitawala sana nyumbani baba alimkubalia mama kwamba Maria aondoke nyumbani na kwenda kusoma katika nyumba ya masista wa Caritas kule Monza. Mikaa pale tangu Machi 1909 mpaka Februari 1913.

Huko walimwita "Valtortino" kwa sababu alijionyesha kuwa na "moyo mkuu, thabiti, imara na mwaminifu". Alipenda masomo, utaratibu mzuri na utii. Wenzake walimnena kuwa “mfano”. Baadaye mama yake alimshurutisha kuchagua masomo ya elimu na habari za ufundi kwa sababu hakupenda hesabu. Alimaliza na mitihani bora ingawa kadiri ya kipaji chake angalikuwa zaidi kusoma na kuandika vitabu vya ufasaha.

Kabla ya kuingia kwenye chuo hiki - aliogopa kupaacha mahali pa amani - alifanya bado mafungo mazuri kusudi ajipatie namna bora ya kuongozwa nayo katika maisha yanayokuja: akuze utu wake. Na Bwana hakukosa kujionyesha kwake mara ya pili ili "aelewe kuishi ndani Yake na kwa ajili Yake na pamoja naye”.

Mnamo mwaka 1913 waliamia Firenze baba akipata kujiuzulu kikazi. Maria mara nyingi alikwenda na baba mjini waone nyumba ama sanamu zu kumbukumbu. Kwa binafsi yeye aliendelea vizuri kama wakati alipokuwa shuleni. Mama yake alimzuia alivyoweza na kutaka”afanye uzembe upande wa dini “.

IX

Pale Firenze Maria alimkuta Roberto, kijana mzalendo wa Bari. Akawa mwema, tajiri, na alikuwa amemaliza masomo ya elimu ya vitabu. Mama wa Maria hakutaka wapendane.

Vile vile miaka tisa baadaye alimzuia Maria na kumharibu urafiki wake na mwanaume mwingine Mario.

Lakini Maria hakuweza kuishi bila mapendo. Sasa alipoona kwamba “kupendana kwa njia ya maumbile kunapita “ alitamani kumwendea Mungu.

Ndoto ya kubashiri. Huduma ya nesi. Kupigwa viunoni

Kuanzia mwaka 1916 - Maria alihuzunika na kumtamani sana Mungu - Mungu alimpa ndoto ambayo Maria hakuisahau maishani kamwe: Yesu alimwangaza na kumbariki atakaswe.

Hiyo ndoto itakuwa kwake kama ubashiri wa kazi yake ya baadaye ya mwandishi wa habari za kienjili.

Maria hakufahamu zaidi wakati ule na 1917 akaenda kuwa mwuguzi katika hospitali ya wanajeshi pale Firenze kwa miezi kumi na minane. Alitaka “kuwasaidia wagonjwa lakini siyo kumtafuta mchumba”.

Alijisikia ampende Mungu daima zaidi. Mwanzo huo huo wa kujitolea kwa Mungu ndio mwanzo wa maradhi yake:

Tarehe 17 Machi 1920 alipotembea na mama yake barabarani Maria alipigwa vibaya ghafula na mtoto mmoja mtundu. Alimpa pigo la chuma kigumu viunoni. Akalazwa kitandani kwa miezi mitatu.

Maisha ya roho na kujitolea dhabihu

Oktoaba ya mwaka ulej jamaa wakaenda Reggio Calabria kwa ndugu Belfanti wenye mahoteli mengi kidogo.

Kule Maria alisoma kitabu 'Mtakatifu' kilichoandikwa na Antonio Fogazzaro. Kilimpa wazo sana. Alianza kuvutwa sana na maisha ya Mtakatifu Franzisko wa Assisi na ya Teresia wa Mtoto Yesu. Alianza kujiona kama kuna ukweli nje ya kawaida. Zamani pia alidhani ni "kutambua mbeleni matokeo yanayofuata". Hasa aliamini kwamba kutoka vidoleni vyake nyuzi zinaelekea nje angani zinapounganika na nyuzi za watu wengine kama kutafuta ushirikiano. Mwanzoni mwa mwezi wa Agosti 1922 walirudi tena Firenze na katika Septemba 1924 walihamia kabisa Viarejo katika kinyumba walichonunua. Sasa alianza maisha ya kiroho rasmi. Wakati wa matembezi yake huzoea kwenda kuabudu sakramenti ya Ekaristi Takatifu "bila mama yake kumwonea vibaya".

Kadiri ya mfano wa Mtakatifu Teresia wa Mtoto Yesu ambaye kitabu chake 'Hadithi ya moyo nafsi mmoja' alikuwa amesoma akajitolea Kwake Ndiye Upendo wa Huruma 28 Januari 1925. Kila siku alirudia majitoleo hayo. Mapendo kwa Yesu yalizidi. Katika maneno na matendo yake aknmtambua Bwana Yesu kuwa karibu naye.

Mateso, fidia na upendo.

Utume wa pekee wa kuwa mwandishi wa mambo ya kiroho

Maria akataka kujiunga na Shirika la Mtakatifu Paulo. Hakuweza na ikambidi kuwa na utume uliofahamika na Mungu peke Yake tu na uliokuwa hasa wa mateso.

X

Lakini katika mwezi wa Desemba akateuliwa kuwa mwongozi wa elimu kwa ajili ya vijana katika Aksio Katoliki. Hivyo sasa aliweza kuja miongoni mwa watu na kuwasaidia kiroho na kuwahubiria. Walikuja watu wengi sana na pia walioasi.

Aliweka tena nadhiri kali zaidi mbele ya Mungu tarehe 1 Julai 1931. Kutoka hapo hakuwa tena bila mateso: mara ya mwisho ya kuweza kutoka nyumbani kwa kujikaza kabisa ilikuwa tarehe 4 Januari 1933. Tangu tarehe 1 Aprili 1934 ilimbidi kulala kitandani daima na akaanza kuugua kwa muda mrefu na vibaya mno. Lakini siyo bure. Alijaliwa "akiwa na nia kuu kwa kujitolea kwa mapendo yanayofurika".

Akawa 'chombo' mikononi mwa Mungu. Utume wake ulikuwa "mateso, fidia na upendo".

24 Mai 1935 Marta Diciotti alifika. Atakuwa mfariji wa Maria, "msikilzaji" wa maandiko yake, mwuguzi na msaidizi mpendwa mpaka kifo cha Maria na baadaye mlinzi wa wingi wa kumbusho zake.

Lakini mara ukaja msiba wa baba yake tarehe 30 Juni 1935 uliomletea uchungu sana.

"Alitimiza wajibu zake na ustahimilivu na wema. Alisamehe waliomtia uchungu na alifidia ubaya kwa wema. Alijishinda kuwaendea vizuri waliomchukiza na wasiofahamu nia yake bora".

Maria aliteseka na kujuta kwamba hakuweza kumsaidia katika masaa yake kabla ya kifo na kutokumwona jenezani. Alipelekwa katika mipaka ya mauti na maisha kwa ajili hiyo.

Mama yake akageuka kuwa mkali zaidi na mtawala "baada ya michezo mipumbavu michache ya upendo wake uliochelewa". Alitaka kuwa mkubwa yeye peke yake tu.

Na Maria akaendelea na mateso kitandani na kupenda na akazidi kumtii Mungu. Akawatuliza wenye uchungu. Akainusha waliopotea kiroho. Akazona mbeleni na kuumia kwa ajili ya masaa yenye giza. Kwa nyakati hizo alikuwa daima na moyo mkuu na roho ya kumwamini Mungu. Padre Migliorini mtawa wa Watumishi wa Bikira Maria alimwomba kuandika hadithi ya maisha yake, iliyomfanya "aweze kuongea juu ya mazuri mabaya" kutoka moyo wazi.

Kazi yake rasmi ya mwandishi Maria alipata kutokana na mwaliko kuoka juu. Alijibu kwa kutii awe chombo cha kutumiwa na mbingu. Ikawa mnamo mwaka 1944, wakati wa vita vikuu vya kuogofya, Alijaza kurasa za daftari elfu kumi na tano bila misaada ya vifaa bora na akipata mateso mengi katika hali zisizofaa kabisa kibinadamu.

Siku hizi tu maandiko hayo yametambulika na kubaliwa kuwa ukumbusho mkuu wa mafundisho ya dini na ya ufasaha wa lugha.

Maisha yake Maria yateketea, kifo na kaburi lake

18 Aprili 1949 Maria alimtolea Mungu nia ya kutokutaka kazi ikubaliwe na kanisa kabla ya kifo chake. Pia alitaka kumtolea Mungu akili yake.

Mungu alikubali: baada ya kusikia kwamba vitabu vimeahirishwa Maria akaingizwa kwenye upweke rohani hasa kutoka mwaka 1956.

Baadaye ameonekana na upungufu wa akili akianza kuandika na herufi kubwa mara nyingi mno. Pia alitaka kujaza kila kikaratasi na maandiko.

Hata picha akazijaza na sala.

XI

Wakati bila kazi alionekana macho na mtulivu. Lakini kwa waliokuja kuongea alijibu vitu visivyoeleweka ama alirudia tu maneno ya mwisho, mazungumzo hayakuwezekana tena. Pengine akatoa milio mifupi ama mirefu sana ama huweza kusema: "Je, jua linawakaje hapal".

Lazima alitunzwa kama mtoto mkubwa. Lakini hakuomba chochote. Nyumbani alibaki tu Marta Diciotti, baada ya kifo cha mama yake katika mwaka 1943. Wakaja wageni wachache tu kama marafiki kwa shida.

12 Oktoba 1961 Maria alifariki kimya wakati wa mwaka wa sitini na tano kutoka azaliwe na mwaka wa ishirini na nane wa kulala mgonjwa kitandani.

Katika mwandiko wake mmoja tunasoma kwamba Bwana alimwambia: "Utakuwa na furaha kubwa sana nitakapokuchukua ndani ya ulimwengu wangu kwa milele kutoka dunia hiyo maskini. Hukuwa umekubalia dunia hiyo kabisa. Utakwenda kutoka maono yako mpaka ndani ya hali ya ukweli kama mdogo anayemwona mama yake kwa ndoto, angeamka kabisa, na mama yake angemkumbatia. Hivyo hivyo itakuwa". Padre Innocenzo Maria Rovetti mkuu wa utawa wa tatu wa Watumishi wa Maria alitwa kwa kifo cha Maria. Maria alikuwa mshiriki wa jamii na pia wa Mtakatifu Franzisko. Padre alimwambia sala kumfariji, alisema: "Roho kikristu uage na dunia hiyo". Maria aliinamisha kichwa chake na kutoa pumzi la mwisho kama angalitii tena mara ya mwisho.

Maiti yake ililazwa katika chumba kile kile ambamo alikaa muda mrefu na kuvumilia mateso mengi. Pia walimtandazia shela yake iliyokuwa ya ubatizo kichwani pamoja na picha iliyotayarishwa naye kabla yenye maneno haya: "Nimemaliza kuteseka lakini nitaendelea kupenda". Wageni wengine waliokuja kwa msiba walidhani kuona

mkono wake wa kulia umeng'aa kidogo kuliko ule wa kushoto: maana ule wa kulia ulitumika sana kama "kalamu ya Bwana". Mwili ilinyoka lakini magoti yalikuwa yamejikunja kidogo. Yalikuwa meza yake ya kuandikia. Wakachukua sura ya uso wake.

14 Oktoba alizikwa kimya baada ya misa takatifu. Baada ya miaka kumi tena wakamtengeneza na kuweka katika hali ya kudumu. Akawekwa katika kaburi la jamaa yake palepale kwenye shamba la Mungu ile ile.

Lakini tarehe ya 2 Julai 1973 alihamishwa katika kanisa Santissima Annunziata huko Firenze katika mahali pa kuwazika mapadre Watumishi wa Maria,

Injili kama nilivyofunuliwa

Ni maandiko maalum ya mwandishi huyo anamoeleza maisha yake Bwana Yesu, tangu azaliwe Bikira Maria hadi Kupokea kwake mbinguni.

Maandiko haya siyo Injili mpya, lakini ni utimilifu wa yale mapokea manne ya kienjili na ufafanuzi wake. Maria Valtorta aliita kazi hiyo "Habari Njema ya Bwana yetu Yesu Kristu kama Yohane Mdogo alivyofunuliwa". Kufunuliwa maana mwandishi ashuhudia hakuna asili ya kibinadamu alikoweza kupata aandikalo. Yohane maana mara nyingi huitwa hivi na Bwana Yesu, akimfananisha na yule mwandika Injili, mwanafunzi wake mpendwa. Mdogo maana mwandishi akadirika kazi yake ni ya kufuatana na chmi ya ile ya Injili Takatifu.

Kazi nzima imegawika katika taratibu ya pekee ya sura ya kuendelea.

XII

Kila sura imegawiwa katika aya nyingi, kila moja yenye maana yake iliyo-timilika.

Shabaha ya Kazi hii

Shabaha yametolewa na Bwana Yesu mwenyewe katika imla yake mojawapo kwa mwandishi: "Mapenzi yangu ni kwamba Neno langu lijulikane, lienee, litumike na watakatifu na waamini... Ningependa kwamba kutoka Nchi hii... ulimo Ukao wa Kimitume... Kazi ieneze... kwenye ulimwengu wote wa wakristu-katolilki.

Maandiko mengine

Maria Valtorta aliandika vitabu vingine kadhaa, hasa: "Kitabu cha Azaria" (Kielezo cha kiroho na cha teolojia kuhusu Misa ishirini na nane za sikukuu), na "Maisha yake mwenyewe".

XIII

INJILI NNE

ZILIZOUNGANISHWA

zahasika na sura za Kitabu cha kwanza cha "Injili kama nilivyofunuliwa" (*).

DIBADJI

Yn 1:1-18. Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyu mwanzo alikuwako kwa Mungu.

Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo Yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika.

Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu.

Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza.

Palitokea mtu, ametumwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yohane. Huyo alikuja kwa ushuhuda, ili aishuhudie ile nuru wote wapate kuamini kwa yeye. Huyo hakuwa ile nuru, bali alikuja ili aishuhudie ile nuru.

Kulikuwako Nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu. Alikuwako ulimwenguni, hata kwa yeye ulimwengu ulipata kuwako, wala ulimwengu haukumtambua. Alikuwa kwake, wala walio wake hawakumpokea.

Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu.

Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu. kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.

Yohane alimshuhudia, akapaza sauti yake akasema: “Huyo ndiye niliyenena habari zake ya kwamba: ajaye nyuma yangu amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu”.

Kwa kuwa katika utimilifu yake sisi sote tulipokea, na neema juu ya neema. Kwa kuwa torati ilitolewa kwa mkono wa Musa; neema na kweli zilikuja kwa mkono wa Yesu Kristu. Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mungu Mwana pekee aliyekatika kifua cha Baba, huyu ndiye aliyemfunua.

1

Lk 1: 1-4. Kwa kuwa watu wengi wametia mikono kutunga kwa taratibu habari za mambo yale yaliyotimizwa katikati yetu, kama walivyotuhadithia wale waliokuwa mashahidi wenye kuyaona, na watumishi wa lile neno tokea mwanzo, nimeona vema mimi nami, kwa kuwa nimejitafutia usahihi wa mambo hayo yote tangu mwanzo, kukuandikia kwa taratibu, Theofilo mtukufu, upate kujua hakika ya mambo yale uliyofundishwa.

(*) Injili nne zilizounganishwa na Emilio Pisani zimenakiliwa zinapohusika na maandiko ya Maria Valtorta. Kama Injili zinaambatana, maneno yaonyesha tu Injili ya kwanza kati yao, jinsi ilivyo, na kukamilishwa kwa sehemu mpya za Injili zingine, zinazolingizwa katika vifungo vya mraba, hivi (). Tarakimu kubwa zaonyesha sura za “Injili kama nilivyofunuliwa”; zikiwa ndani ya maandiko ya Injili, kama vile 1 na 2-15, maana yake hakuna uhusiano wake na aya za Injili Takatifu, utika si kitu utaratibu wa habari zilivyotimizwa.

Sura za Injili nne zilionakiliwa zimetoka katika “Biblia” United Bible Societies, 1989.

XIV

UTOTO WAKE BWANA YESU

2-15

Lk. 1: 5-25. Zamani za Herode, mfalme wa Uyahudi, palikuwa na kuhani mmoja, jina lake Zakaria, wa zamu ya Abiya, na mkewe alikuwa mmojawapo wa uzao wa Haruni jina lake Elisabeti. Na wote wawili walikuwa wenye haki mbele za Mungu, wakiendelea katika amri zote za Bwana na maagizo yake bila lawama. Nao walilikuwa hawana mtoto, maana Elisabeti alikuwa tasa, na wote wawili ni wazee sana.

Basi ikawa, alipokuwa akifanya kazi ya ukuhani katika taratibu ya zamu yake mbele za Mungu, kama ilivyokuwa desturi ya ukuhani, kura ilimwangukia kuingia katika hekalu la Bwana ili kufukiza uvumba. Na makutano yote ya watu walikuwa wakisali nje saa ya kufukiza uvumba. Akatokewa na malaika wa Bwana, amesimama upande wa kuume wa madhabahu ya kufukizia. Zakaria alipomwona ali-

fadhaika, hofu ikamwingia.

Lakini yule malaika akamwambia: “Usiogope, Zakaria, maana dua yako ime- sikiwa, na mkeo Elisabeti atakuzalia mtoto mwanamume, na jina lake utamwita Yohane. Nawe utakuwa na furaha na shangwe, na watu wengi watakufurahia kuzaliwa kwake. Kwa sababu atakuwa mkuu mbele za Bwana; hatakuunywa divai wala kileo; naye atajazwa Roho Mtakatifu hata tangu tumboni mwa mamaye. Na wengi katika Waisraeli atawarejeza kwa Bwana Mungu wao. Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya, na nguvu zake, ili kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na kuwatilia waasi akili za wenye haki, na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa”.

31-7 Zakaria akamwambia malaika: “Nitajuaje meno hilo? maana mimi ni mzee, na mke wangu ni mkongwe wa siku nyingi”. Malaika akamjibu akamwambia: “Mimi ni Gabrieli, nisimamaye mbele za Mungu; nami nimetumwa niseme nawe, na kuku- 21-4 pasha habari hizi njema. Na tazama! utakuwa bubu, usiweze kusema, mpaka 21-6 siku ile yatakapotukia hayo, kwa sababu hukuyasadiki maneno yangu; nayo 25-2 yatatimizwa kwa wakati wake”

Na wale watu walilikuwa wakimngojea Zakaria, wakastaajabia kukawia kwake mle hekaluni. Alipotoka hali hawezi kusema nao, walitambua ya kuwa amœna maono ndani ya hekalu, naye aliendelea kuwaashiria akakaa bubu.

Ikawa siku za huduma yake zilipokuwa zimetimia akaenda nyumbani kwake. Hata baada ya siku zile mkewe Elisabeti alichukua mimba akatawa miezi mitano, akisema: “Hivi ndivyo alivyotendea Bwana katika siku zile alizoniangualia ili kuniondolea aibu yangu mbele ya watu”.

Lk. 1: 26-38. Mwezi wa sita, malaika Gabrieli alitumwa na Mungu 16 kwenda mpaka mji wa Galilaya, jina lake Nazareti, kwa mwanamwali bikira aliyekuwa ameposwa na mtu, jina lake Yusufu, wa mbari ya Daudi; na jina lake bikira huyo ni Maria. Akaingia nyumbani kwake akasema: “Salamu, uliyepewa neema, Bwana yu pamoja nawe”. Naye akafadhaika sana kwa ajili ya maneno yake, akawaza moyoni, Salamu hii ni ya namna gani? Malaika akamwambia: “Usiogope, Maria, kwa maana umepata neema kwa Mungu. Tazama utachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume; najina lake utamwita Yesu. Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi, baba yake. Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho”.

Maria akamwambia malaika: “Litakuwaje neno hili, maana sijui mume?”. Malaika akajibu akamwambia “Roho Mtakatifu atakujilia juu yako, na nguvu zake Aliye juu zitakufunika kama kivuli; kwa sababu hiyo hicho kitakachozaliwa ki-XV

taitwa kitakatifu, Mwana wa Mungu. Tena, tazama, jamaa yako Elisabeti naye amechukua mimba ya mtoto mwanamume katika uzee wake; na mwezi huu ni wa sita kwake yeye aliyetwa tasa; kwa kuwa hakuna neno lisilowezezana kwa Mungu”. Maria akasema: “Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu kama ulivyosema”. Kisha malaika akaondoka akaenda zake.

17-18

Lk. 1: 39-55. Basi, Maria akaondoka siku hizo, akaenda hata 19-21 nchi ya milimani kwa haraka mpaka mji mmoja wa Yuda, akaingia nyumbani kwa Zakaria akamwambia Elisabeti. Ikawa Elisabeti aliposikia kule 45.6 kuamkia kwake Maria, kitoto kichanga kikaruka ndani ya tumbo lake; Elisabeti 127.5.. akajazwa Roho Mtakatifu; akapaza sauti kwa nguvu akasema: “Umebarikiwa wewe katika wanawake, naye mzao wa tumbo lako amebarikiwa. Limenitokeaje neno hili, hata mama wa Bwana wangu anijilie mimi? Maana sauti ya kuamkia kwako ilipoingia masikioni mwangu, kitoto

kichanga kikaruka kwa shangwe ndani ya tumbo langu. Naye heri aliyesadiki; kwa maana yatatimizwa aliyoambiwa na Bwana.”.

Maria akasema: “Moyo wangu wamwadhjisha Bwana, na roho yangu imemfurahia Mungu, Mwokozi wangu; kwa kuwa ameutazama unyonge wa mjakazi wake; kwa maana. tazama, tokea sasa vizazi vyote wataniita mbarikiwa; kwa kuwa Mwenye nguvu amenitendea makuu, na jina lake ni takatifu. Na rehema zake hudumu vizazi hata vizazi kwa hao wanaomcha. Amefanya nguvu kwa mkono wake; amewatawanya walio na kiburi katika mawazo ya mioyo yao; amewaangusha wakuu katika viti vyao vya enzi; na wanyonge amewakweza. Wenye njaa amewashibisha mema, na wenye mali amewaondoa mikono mitupu, Amemsaidia Israeli, mtumishi wake; ili kukumbuka rehema zake; kama alivyowaambia baba zetu, Ibrnhimu na uzao wake hata milele”.

Lk. 1: 56. Maria Akakaa naye kadiri ya miezi mitatu, kisha akarudi 22
25.7 kwenda nyumbani kwake.

Lk 1: 57-58. Ikawa, siku za kuzaa kwake Elisabeti zilipotimia, alizaa mtoto 23 mwanamume.
Wakasikia jirani zake na jamaa zake ya kwamba Bwana amemwongezea rehema zake, wakafurahi pamoja naye.

Lk. 1: 59-79. Ikawa siku ya nane wakaja kumtahiri mtoto; wakataka 24
kumpa jina la babaye, Zakaria. Mamaye akajibu akasema: “La, sivyo; bali, ataitwa Yohane”. Wakamwambia: “Hapana mtu katika jamaa zako aitwaye jina hilo.”
Wakamwashiria babaye wajue atakavyo kumwita. Akataka kibao, akaandika ya kwamba: “Jina lake ni Yohane”. Wakastaajabu wote. Papo hapo kinywa chake kikafunguliwa na ulimi wake pia, akaanza kunena akimsifu Mungu. Wakaingiwa na hofu wote waliokuwa wakikaa karibu nao; na mambo hayo yote yakatangazwa katika nchi yote ya milima milima ya Uyahudi. Na wote walioyasikia wakayaweka mioyoni mwao, wakisema: “Mtoto huyu atakuwa wa namna gani? Kwa sababu mkono wa Bwana ulikuwa panoja naye”.

Na Zakaria, baba yake, akajazwa Roho Mtakatifu, akatabiri, akisema: “Atukuzwe Bwana, Mungu wa Israeli, kwa kuwa amewajia watu wake, na kuwakomboa. Ametusimamishia pembe ya wokovu katika mlango wa Daudi, mtumishi wake. Kama alivyosema tangu mwanzo kwa kinywa cha manabii wake watakatifu; tuokolewe na adui zetu na mikononi mwao wote wanaotuchukia; ili kuwatendea rehema baba zetu, na kulikumbuka agano lake takatifu; uapo aliomwambia Ibrahimu, baba yetu, ya kwamba atatujalia sisi, tuoko mikononi mwa adui zetu,
XVI

na kumwabudu pasipo hofu, kwa utakatifu na kwa haki mbele zake siku zetu zote. Nawe, mtoto, utaitwa nabii wake Aliye juu, kwa maana utatungulia mbele za uso wa Bwana umtengenezee njia zake; uwajulishe watu wake wokovu, katika kusamehewa dhambi zao. Kwa njia ya rehema za Mungu wetu, ambazo kwa hizo mwangaza utokao juu umetufikia, kuwaangaza wakao katika giza na uvuli wa mauti, na kuiongoza miguu yetu kwenye njia ya amani”.

25

31.1 Lk. 1: 80. Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu rohoni, akakaa majangwani 45. ½ hata siku ya kutokea kwake kwa Israeli.

Mt 1: 1-17. Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristu, mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahimu.

Ibrahimu alimzaa Isaka; Isaka akamzaa Yakobo; Yakobo akamzaa Yuda na ndugu zake; Yuda akamzaa Peresi na Zera kwa Tamari; Peresi akamzaa Esromu; Esromu akamzaa Aramu; Aramu akamzaa Aminadabu; Aminadabu akamzaa Nashoni; Nashoni akamzaa Salmoni.

209.7 Salmoni akamzaa Boazi kwa Rahabu; Boazi akamzaa Obedi kwa Ruthu; Obedi akamzaa Yese; Yese akamzaa mfalme Daudi.

Daudi akamzaa Sulemani kwa yule mke wa Uria; Sulemani akamzaa Rehoboamu; Rehoboamu akamzaa Abiya; Abiya akamzaa Asa; Asa akamzaa Yehoshafati; Yehoshafati akamzaa Yoram; Yoram akamzaa Uzia; Uzia akamzaa Yothamu; Yothamu akamzaa Ahazi; Ahazi akamzaa Hezekia.

Hezekia akamzaa Manase; Manase akamzaa Amoni; Amoni akamzaa Yosia; Yosia akamzaa Yekonia na ndugu zake wakati wa ule uhamisho wa Babeli.

Na baada ya ule uhamisho wa Babeli, Yekonia akamzaa Shealtieli; Shealtieli akamzaa Zerubabeli; Zerubabeli akamzaa Abihudi; Abihudi akamzaa Eliakimu; Eliakimu akamzaa Azori; Azori akamzaa Sadoki; Sadoki akamzaa Akimu; Akimu akamzaa Eliudi; Eliudi akamzaa Eleazari; Eleazari akamzaa Matani; Matani akamzaa Yakobo; Yakobo akamzaa Yusufu mumewe Maria aliyemzaa Yesu aitwaye Kristu.

Basi vizazi vyote tangu Ibrahimu hata Daudi ni vizazi kumi na vinne; na tangu Daudi hata ule uhamisho wa Babeli ni vizazi kumi na vinne; na tangu ule uhamisho wa Babeli hata Kristu ni vizazi kumi na vinne.

Mt. 1: 18-25. Kuzaliwa kwake Yesu Kristu kulikuwa hivi. Maria mama 26

yake alipopkuwa ameposwa na Yusufu, kabla hawajakaribiana, alionekana
16. 4 ana mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye Yusufu, mumewe, kwa vile
25.10: alivyokuwa mtu wa haki, asitake kumwaibisha, aliazimu kumwacha kwa siri.
Basi alipokuwa akifikiri hayo, tazama, malaika wa Bwana alimtokea katika ndoto, akisema:
“Yusufu, mwana wa Daudi, usihofu kumchukua Maria mkeo, maana mimba
yake ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina
lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao”. Hayo yote
yamekuwa, ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii akisema:
“Tazama, bikira atachukua mimba, naye atazaa mwana; nao watamwita jina lake Imanueli, yaani,
Mungu pamoja nasi”. Naye Yusufu alipoamka katika usingizi, alifanya kama malaika wa Bwana alivyomwagiza, akamchukua mkewe; asimjue
kamwe hata alipomzaa mwanawe; akamwita jina lake Yesu.

Lk. 2: 1-3. Siku zile amri ilitoka kwa Kaisari Augusto ya kwamba iandikwe orodha ya majina ya watu wote wa ulimwengu. Orodha hii ndiyo ya XVII 27

kwanza iliyoandikwa hapo Kirenio alipokuwa liwali wa Shamu. Watu wote wakaenda kuandikwa, kila mtu mjini kwao.

Lk. 2: 4-5. Yusufu naye aliondoka Galilaya, toka mji wa Nazareti, akapanda kwenda Uyahudi mpaka mji wa Daudi, uitwao Bethlehemu, kwa kuwa yeye ni wa mbari na jamaa ya Daudi; ili aandikwe pamoja na Maria mkewe, ambaye amemposa, naye ana mimba. 28

Lk. 2: 6-7. Ikawa, katika kukaa huko, siku zake za kuzaa zikatimia, 29
28 4 akamzaa mwanawe, kifungua mimba, akamvika nguo za kitoto, akamlaza

73.10/11 katika hori ya kulia ng'ombe, kwa sababu hawakupata nafasi katika nyumba ya wageni.

Lk. 2:8-20 Na katika nchi ile ile walikuwako wachungaji wakikaa makondeni na kulinda kundi lao kwa zamu usiku. Malaika wa Bwana akawatokea ghafula, utukufu wa Bwana ukawang'aria pande zote, wakaingiwa na hofu kuu. Malaika akawaambia: "Msiogope; kwa kuwa mimi ninawaletea habari njema ya furaha kuu itakayokuwa kwa watu wote: maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa, kwa ajili yenu, Mwokozi ndiye Kristu Bwana. Na hii ndiyo ishara kweni: mtakuta mtoto mchanga amevikwa nguo za kitoto, amelala katika hori ya kulia ng'ombe" Mara walikuwapo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbinguni, wakimsifu Mungu, na kusema: "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia".

Ikawa, malaika hao walipoondoka kwenda zao mbinguni, wale wachungaji waliambiana: "Haya, na twendeni mpaka Bethlehemu, tukalionge hilo lililofanyika, alilitujulisha Bwana". Wakaenda kwa haraka wakamkuta Maria na Yusufu, na yule mtoto mchanga amelala horini. Walipomwona wakatoa habari waliyoambiwa juu ya huyo mtoto. Wote waliosikia wakastajabu kwa hayo waliyoambiwa na wachungaji. Lakini Maria akayaweka maneno hayo yote, akiyafikiri moyoni mwake. Wale wachungaji wakarudi, huku wanamtukuza Mungu na kumsifu kwa mambo yote waliyosikia na kuyaona, kama walivyoambiwa.

31

Lk. 2: 8-21 Hata zilipotimia siku nane za kumtahiri, aliitwa jina lake Yesu; kama 16.4 alivyoitwa na malaika kabla hajachukuliwa mimba.

Lk. 2: 22-38. Kisha, zilipotimia siku za kutakasika kwao, kama ilivyo torati ya Muga, walikwenda naye hata Yerusalemu, wamweke kwa Bwana, (kama ilivycandikwa katika sheria ya Bwana: gKila mtoto mwanamume aliye kifungua mimba ya mamaye na aitwe mtakatifu kwa Bwanah), wakatoe na sadnka, kama ilivyonenwa katika sheria ya Bwana, hua wawili au makinda ya njiwa wawili.

Na tazama, pale Yerusalemu palikuwa na mtu, jina lake Simeoni, naye ni mtu mwenye haki, mcha Mungo akiitarajia faraja ya Israeli, na Roho Mtakatifu alilikuwa juu yake. Naye alikuwa ameonywa na Roho Mtakatifu ya kwamba hataona mauti kabla ya kumwona Kristu wa Bwana. Basi akaja hekaluni ameongozwa na Roho; na wale wazazi walipomleta mtoto Yesu ndani, ili wamfanyie kama ilivyokuwa desturi ya sheria, yeye mwenyewe alimpokea mikononi mwake, akamshukuru Mungu, akisema: "Sasa, Bwana, wamruhusu mtumishi wako, kwa amani, kama ulivyosema; kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu wako, ulioweka tayari machoni pa watu wote; Nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa, na kuwa utukufu wa watu wako Israeli".

Na babaye na mamaye walikuwa wakiyastajabia hayo yaliyonenwa juu yake.

XVIII

Simeoni akawabariki akamwambia Mada mama yake: "Tazama, huyu amewekwa kwa kuanguka na kuinuka kwa wengi walio katika Israeli, na kuwa ishara itakayonenewa. Nawe mwenyewe, upanga utaingia moyoni mwako, ili yafunuliwe mawazo ya mioyo mingi".

Palikuwa na nabii mke, jina lake Ana, binti Fanueli, wa kabila ya Asheri, na umri wake ulikuwa miaka mingi, alikuwa amekaa na mume miaka saba baada ya uanawali wake. Naye ni mjane wa miaka themanini na minne; haondoki katika hekalu, ila huabudu usiku na mchana kwa kufunga na kuomba. Huyu alitokea saa ile ile akamshukuru Mungu, na wote waliokuwa wakiutarajia ukombozi katika Yerusalemu akawatolea habari zake.

Mt. 2: 1-12. Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashariki walifika Yerusalemu, wakisema: “Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia”. Basi mfalme Herode aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye. Akakusanya wakuu wa makuhani wote na waandishi wa watu akatafuta habari kwao: “Kristu azaliwa wapi?”. Nao wakamwambia: << “Katika Bethlehemu ya Uyahudi; kwa maana ndivyo iliyoandikwa na nabii: “Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Yuda, hu mdogo kamwe kataka majumbe wa Yuda; kwa kuwa kwako atatoka mtawala atakayewachunga watu. wangu Israeli”>>:

Kisha Herode akawaita wale mamajusi faragani, akapata kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota. Akawapeleka Bethlehemu, akasema: “Shikeni njia, mkaulize sana mambo ya mtoto; na mkiisha kumwona, nileteeni habari, ili mimi nami niende nimsujudie”.

Nao waliposikia maneno ya mfalme, walishika njia; na tazama ile nyota waliyoiona mashariki ikawatangulia, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto. Nao walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kubwa mno. Wakaingia nyumbani, wakamwona mtoto pamoja na Maria mamaye, wakaanguka wakamsujudia; nao walipokwisha kufungua hazina zao, wakamtotea tunu; dhahabu na uvumba na manemane.

Nao wakiisha kuonywa na Mungu katika ndoto wasimrudie Herode, wakaenda zao kwao kwa njia nyingine.

Mt. 2: 13-15. Na hao walipokwisha kwenda zao, tazama, malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto, akasema: “Ondoka, umchukue mtoto na mama yake, ukimbilie Misri, ukae huko hata nikuambie; kwa maana Herode anataka kumtafuta mtoto amwangamize”. Akaondoka akamchukua mtoto na mama yake usiku, akaenda zake Misri; akakaa huko hata alipokufa Herode: ili litimie neno lililonenwa na Bwana kwa ujumbe wa nabii, akisema: “Kutoka Misri nalimwita mwanangu”.

Mt. 2: 16-23. Ndipo Herode, alipoona ya kuwa amedhihakiwa na wale mamajusi, alighadhibika sana, akatuma watu akawaua watoto wote wanaume waliokuwako

41.5 huko Bethlehemu na viungani mwake mwote, tangu wenye miaka miwili na walio- 73.2/7 pungua, kwa muda ule aliouhakikisha kwa wale mamajusi. Ndipo lilipotimia neno 74.3/8tab lililonenwa na nabii Yeremia, akisema: “Sauti ilisikiwa Rama, kilio na 75.2/4 maombolezo mengi, Raaheli akiwalilia watoto wake, asikutbali kufarijiwa, kwa kuwa hawako”. Hata alipofariki Herode, tazama, malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto huko Misri, akasema: “Ondoka, umchukue mtoto na mamaye, ushike njia kwenda nchi ya Israeli; kwa maana wamekufa walioitafuta roho ya mtoto”. Aknon- XIX

doka akamchukua mtoto na mamaye, akafika nchi ya Israeli. Lakini aliposikia ya kwamba Arkelao anamiliki huko Urahudi mahali pa Herode babaye, aliogopa kwenda huko; naye akiisha kuonywa katika ndoto, akasafiri pande za Galilaya, akaenda, akakaa katika mji ulioitwa Nazareti; ili litimie neno lililonenwa na manabii: "Ataitwa Mnazareti".

Lk. 2: 39-40. Basi, walipokwisha kuyatimiza yote kama yalivyoagizwa katika sheris ya Bwana, walirejea Galilaya mpaka mjini kwao, Nazareti. Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa heltima, na neema ya Mungu ilikuwa juu yake.

Lk. 2: 41-50. Basi, wazee wake huenda Yerusalemu kila mwaka, wakati wa sikukuu ya Pasaka. 41

Na alimpata umri wake miaka kumi na miwili, walipanda kama ilivyokuwa desturi ya sikukuu; na walipokwisha kuzitimiza siku, wakati wa kurudi kwao, yule mtoto Yesu alibaki nyuma huko Yerusalemu, na wazee wake walikuwa hawana habari. Nao wakadhani ya kuwa yumo katika msafara; wakaenenda mwendo wa kutwa, wakawa wakimtafuta katika jamaa zao na wenzao; na walipomkosa, wakarejea Yerusalemu: huku wakimtafuta. Ikawa baada ya siku tatu wakamwona hekaluni, ameketi katikati ya waalimu, akiwasikiliza na kuwauliza maswali. Nao wote 136.10 waliomsikia walistaajabia fahamu zake na majibu yake. Na walipomwona walishangaa, ra mama yake akamwambia: "Mwanangu, mbona umetutenda hivi Tazama, baba yako na mimi tulikuwa tukikufuta kwa huzuni" Akawaambia: "Kwani kunitafuta? Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?" Nao hawakuelewa na neno hilo alilowaambia.

Lk.2: 51-52. Akashuka pamoja nao mpaka Nazareti, naye alikuwa akiwatii; na 41.12 mamaye aliyaweka hayo yote moyoni mwake. Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu.

42-44

MAISHA YA BWANA YESU WAZI KWA WATU

Mt. 1: 1. Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristu, Mwana wa Mungu.

Lk. 3: 1-2. Mwaka wa kumi na tano wa kutawala kwake Kaisari Tiberio, Pontio Pilato alipokuwa liwali wa Uyahudi, na Herode mfalme wa Galilaya, na Filipo, ndugu yake, mfalme wa Iturea na nchi ya Trakoniti, na Lisania mfalme wa Abilene, wakati wa ukuhani mkuu wa Anasi na Kayafa, neno la Mungu lilimfikia Yohane, mwana wa Zakaria, jangwani.

Yn. 1:19-28. Na huu ndio ushuhuda wake Yohane, wayahudi walipotuma kwake makuhani na Walawi kutoka Yerusalemu ili wamwulize: "Wewe u nani?". Naye alikiri, wala hakukana; alikiri kwamba: "Mimi siye Kristo" Wakamwuliza: XX

“ Ni nini basi? U Eliya wewe?”. Akasema: “Mimi siye”. “Wewe u nabii yule?”. Akajibu: “La”. Basi wakamwambia: “U nani? tuwape majibu wale waliotupeleka. Wanenaje juu ya nafsi yako?”. Akasema: “Mimi ni sauti ya mtu aliaye nyikani, Inyosheni njia ya Bwana! kama vile alivyonena nabii Isaya”. Nao wale waliotumwa walikuwa wametoka kwa Mafarisayo. Wakamwuliza, wakamwambia: “Mbona basi wabatiza, ikiwa wewe si Kristu, wala Eliya, wala nabii yule?”. Yohane akawajibu akisema: “Mimi nabatiza kwa maji. Katikati yenu amesimama yeye msiyemjua ninyi. Ndiye yule ajaye nyuma yangu, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya kiatu chake”.

Hayo yalifanyika huko Bethania ng'ambo ya Yordani, alikokuwako Yohane akibatiza.

Mt. 3: 1-17 [Mk. 1: 2-11; Lk. 3: 3-17 na 21-22] . Siku zile aliondokea 45
Yohane Mbatizaji akihubiri katika nyika ya Uyahudi, na kusema: “Tubuni;

kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. Kwa sababu huyo ndiye aliyenenwa na nabii Isaya, akisema: “[Tazama, namtuma mjumbe wangu mbele ya uso wako, atakayeitengeneza njia yako.] Sauti ya mtu aliaye nyikani: Itengenezeni njia ya Bwana, yanyosheni mapito yake [Kila bonde litajazwa, na kila mlima na kilima kitashushwa; palipotoka patakuwa pamenyoka, na palipoparuza patalainishwa, na wote wenye mwili watauona wokovu wa Mungu.]”>>.

Naye Yohane mwenyewe alikuwa na vazi lake la singa za ngamia, na mshipi wa ngozi kiunoni mwake; na chakula chake kilikuwa nzige na asali ya mwitu. Ndipo walipomwendea Yerusalemu, na Uyahudi wote, na nchi zote za kandokando ya Yordani; naye akawabatiza katika mto wa Yordani, huku wakiziungama dhambi zao.

[Makutano wakamwuliza: “Tufanye nini basi?”. Akawajibu akiwaambia: “Mwenye kanzu mbili na ampe asiye na kanzu; na mwenye vyakula na afanye vivyo hivyo”. Watoza ushuru nao wakaja kubatizwa, wakamwuliza: “Mwalimu, tufanye nini sisi?”. Akawaambia: “Msitoe kitu zaidi kuliko mlivyoamriwa”. Askari nao wakamwuliza, wakisema: “Sisi nasi tufanye nini”. Akawaambia: “Msidhulumu mtu, wala msishitaki kwa uongo; tena mtoshewe na mshahara wenu”.]

Hata alipoona wengi miongoni mwa Mafarisayo na Masadukayo wakujia ubatizo wake aliwaambia: “Enyi wazao wa nyoka, ni nani aliyewaonya ninyi kuikimbia hasira itakayokuja? Basi zaeni matunda yapasayo toba; wala msiwaze mioyoni mwenu kwamba: “Tunaye baba, ndiye Ibrahimu”. Kwa maana nawaambia ya kwa mba Mungu aweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Na shoka limekwisha kuwekwa penye mashina ya miti; basi kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa motoni”.

[Basi watu walipokuwa walingoja yatakayotokea, wote wakiwaza-waza mioyoni mwao habari za Yohane, kama labda yeye ndiye Kristu, Yohane alijibu akawaaambia wote:] “Kweli mimi nawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba; bali yeye ajaye nyuma yangu ana nguvu kuliko mimi, wala sistahili hata kuvichukua viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto. Ambaye pepeto lake li mkononi mwake, naye atausafisha sana uwanda wake, na kuikusanya ngano yake ghalani, bali makapi atayateketeza kwa moto usiozimika”.

Wakati huu Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohane ili abatizwe. Lakini Yohane alitaka kumzuia, akisema: “Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waya kwangu?” Yesu akajibu akamwambia: “Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote” Basi akamkubali, Naye Yesu alipokwisha kubatizwa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema: “Huyu ni Mwanangu mpendwa wangu ninayependezwa naye”.

XXI

Yn. 1: 29-36. Siku ya pili yake amwona Yesu anakuja kwake, akasema: <<Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu! Huyu ndiye niliyenena habari zake ya kwamba, Yuaja mtu nyuma yangu, ambaye amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu. Wala mimi sikumjua; lakini kusudi adhihirishwe kwa Israeli ndiyo maana mimi nalikuja nikibatiza kwa maji”.

47.2 Tena Yohane akashuhudia akisema: “Nimemwona Roho akishuka kama hua 47.10 kutoka mbinguni; naye akakaa juu yake. Wala mimi sikumjua; lakini yeye aliyenipeleka kubatiza kwa maji, huyo aliniambia: “Yeye ambaye utamwona Roho akishuka na kukaa juu yake, huyo ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu”. Nami nimeona, tena nimeshuhudia ya kuwa huyu ni Mwana wa Mungu”

Tena siku ya pili yake Yohane alikuwa amesimama pamoja na wawili katika wanafunzi wake. Akamtazama Yesu akitembea, akasema: “Tazama, Mwana-kondoo wa Mungu”

Lk. 3, 18-20. Basi kwa maonyo mengine mengi aliwahubiri watu. Lakini mfalme Herode alipokaripiwa na yeye kwa ajili ya Herodia, mke wa nduguye, na maovu
47.2 yote aliyoyafanya Herode, aliongeza na hili juu ya yote, alimfunga Yohane gerezani.

Mt. 4: 1-11 [Mk. 1: 12-13 Lk. 4: 1-13] . Kisha Yesu [hali amejaa Roho Mtakatifu, alirudi kutoka Yordani] alipandishwa na Roho nyikani, ili ajari-biwe na Ibilisi [naye alikuwa pamoja na wanyama wa mwitu]. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa.]

Mjaribu akamjia akamwambia: “Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate”. Naye akajibu akasema: “Imeandikwa: Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mugu”.

Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, akamwambia: “Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini; kwa maana imeandikwa: Atakuagizia malaika zake; na mikononi mwao watakuchukua; usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe”. Yesu akamwambia: “ Tena imeandikwa: Usimjaribu Bwana Mungu wako”.

Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake akawambia: “Haya yote nitakupa, [nitakupa wewe enzi hii yote, na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa ye yote kama nipendavyo ukianguka kunisujudia [yote yatakuwa yako]”. Ndipo Yesu alipomwambia: “Nenda zako Shetani; kwa maana imeandikwa: Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye pqke yake”.

Kisha Ibilisi [, alipomaliza kila jaribu] akamwacha; na tazama, wakaja malaika wakamtumikia.

Yn. 1: 37-39. Wale wanafunzi wawili wakamsikia akinena, wakamfuata Yesu. Yesu aligeuka, akawaona wakimfuata, akawaambia: “Mnatafuta ni-ni?” Wakamwambia: “Rabi (maana yake, Mwalimu), unakaa wapi?” Akawaambia: “Njoni, nanyi mtaona”. Wakaenda, wakaona akaapo, wakakaa kwake siku ile. Nayo ilikuwa yapata saa kumi.

47. 2 Mt. 4: 12-17 [Mk. 1: 14-15; Lk. 4: 14] Basi Yesu aliposikia kwamba Yohane amefungwa [kwa nguvu za Roho] alikwenda zake mpaka Galilaya; akatoka Nazareti

48. 7 akaja akakaa Kapernaumu, rnji ulioko pwani, mipakani mwa Zabuloni, na Nahali: ili litimie neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema: “Nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, njia ya bahari, ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya mataifa, watu wale waliokaa katika giza wameona mwanga mkuuo, nao waliokaa katika nchi na uvuli wa mauti mwanga umewazukia”. [habari zake zikaenea katika nchi zote za kandokando].

XXII

49.6 Tekea wakati huo Yesu alianza kuhubiri (Habari Njema ya ufalme wa Mungu),

59.4 na kusema: “(Wakati umetimia) tubuni (na kuiamini Injili) kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia”.

Lk. 3: 23-38. Na Yesu mwenyewe, alipoanza kufundisha, alikuwa amepata umri wake kama miaka thelathini, akidhaniwa kuwa ni mwana wa Yusufu, wa Eli, wa Mathati, wa Lawi, wa Melki, wa Yana, wa Yusufu, wa Matathia, wa Amosi, wa Nahumu, wa Esli, wa Nagai, wa Maathi, wa Matathia, wa Semei, wa Yusufu, wa Yuda, wa Yoana, wa Resa, wa Zerubabeli, wa Shealtieli, wa Neri, wa Melki, wa Adi, wa Kosa-mu, wa Elmadamu, wa Eri, waY oshua, wa Eliezeri, wa Yorimu, wa Mathati, wa Lawi, wa Simeoni, wa Yuda, wa Yusufu, wa Yonamu, wa Eliakimu, wa Melea, wa Mena, wa 209.7

Matatha, wa Nathani, wa Daudi, wa Yese, wa Obedi, wa Boazi, wa Salmoni, wa Nashoni, wa Aminadabu, wa Aramu, wa Hesroni, wa Peresi, wa Yuda, wa Yakobo, wa Isaka, wa Ibrahimu, wa

Tera, wa Nahori, wa Serugi, wa Ragau, wa Pelegi, wa Eberi, wa Sala, wa Kenani, wa Arfaksadi, wa Shemu, wa Nuhu, wa Lameki, wa Methusela, wa Henoko, wa Yaredi wa Mahalaleli, wa Kenani, wa Enoshi, wa Sethi, wa Adamu, wa Mungu

Yw 1: 40-42. Andrea, nduguye Simoni Petro, alikuwa mmoja wa 48- 49 wale wawili waliomsikia Yohane na kumfuata Yesu. Huyu akamwona kwanza Simoni, ndugu yake mwenyewe, akamwambia: “Tumemwona Masiha (maana yake, Kristu”. Akampeleka kwa Yesu. Naye Yesu akamtazama, akasema: “Wewe Simoni, mwana wa Yohane; nawe utaitwa Kefa (tafsiri yake Petro, au liwe”.

Yn. 1: 43-51 Siku ya pili yake alitaka kuondoka kwenda Galilaya, naye 50 akamwona Filipo. Yesu akamwambia: “Nifuate”. Naye Filipo alikuwa mtu wa Bethsaida mwenyeji wa mji wa Andrea na Petro. Filipo akamwona Nathanaeli, akamwambia: “Tumemwona yeye aliyeandikiwa na Musa katika torati, na manabii, Yesu, mwana wa Yusufu, mtu wa Nazareti”. Nathanaeli akamwambia: “Laweza neno jema kutoka Nazareti?. Filipo akamwambia: “Njoo uone”. Basi Yesu akamwona Nathanaeli anakuja kwake, akanena habari zake: “Tazama, Mwisraeli kweli kweli, hamna hila ndani yake”. Nathanaeli akamwambia: “Uumepataje kunitambua”. Yesu akajibu, akamwambia: “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwapo chini ya mtini nililikuona”. Nathanaeli akamjibu: “ Rabi, wewe u Mwana wa Mungu, ndiwe Mfalme wa Israeli”. Yesu akajibu, akamwambia: “Kwa sababu nilikuambia; nilikuona chini ya mtini, waamini? Utaona mambo makubwa kuliko haya”. Akamwambia: “Amin, amin, nawaambia: mtaziona mbingu zimefungka na malaika wa Mungu wakikwea na kushuka juu ya Mwana wa Adamu”.

Yn. 2: 1-11. Na siku ya tatu palikuwa na arusi huko Kana, mji 51 - 52 wa Galilaya; naye mama yake Yesu alikuwapo. Yesu naye alikuwa amealikwa arusini pamoja na wanafunzi wake. Hata divai ilipowatindikia, mamaye Yesu akamwambia: “Hawana divai”. Yesu akamwambia: “Mama, tuna nini mimi nawe? Saa yangu haijawadia”. Mamaye akawaambia watumishi: “Lo lote atakalowambia, fanyeni” Basi kulikuwako huko mabalasi sita ya mawe, nayo yamewekwa huko kwa desturi ya Wayahudi ya kutawadha, kila moja lapata kadiri ya nzio mbili tatu. Yesu akawaambia: "Jalizeni mabalasi maji" Nao wakayajaliza hata juu. Akawaambia: "Sasa tekeni, mkampelekee mkuu wa meza". Wakapeleka. Naye mkuu wa meza alipoyaonya yale maji yaliyopata kuwa divai, (wala asijue ilikotoka, lakini watumishi walijua, wale walioyateka yale maji), yule mkuu wa meza alimwita bwana arusi, akamwambia: "Kila mtu kwanza huandaa divai iliyo nje- XXIII

ma; hata watu wakiisha kunywa sana ndipo huleta iliyo dhaifu; wewe umeiweka divai iliyo njema hata sasa".

Mwanzo huo wa ishara Yesu aliufanya huko Kana ya Galilaya, akaudhihirisha utukufu wake, nao wanafunzi wake wakamwamini.

Yn. 2: 12-25. Baada ya hayo akashuka mpaka Kapernaumu, yeye na ma- 53 ma yake na ndugu zake na wanafunzi wake; wakakaa huko siku si nyingi. Na Pasaka ya Wayahudi ilikuwa karibu; naye Yesu akakwea mpaka Yerusalemu. Akaona pale hekaluni watu waliokuwa wakiuza ng'ombe na kondoo na njiwa, na wenye kuvunja fedha wameketi. Akafanya kikoto cha kambaa, akawatoa wote katika hekalu, na kondoo na ng'ombe; akamwaga fedha za wenye kuvunja fedha, akazipindua meza zao; akawaambia wale waliokuwa waliokuwa njiwa: "Yaondoeni haya; msiifanye nyumba ya Baba yangu kuwa nyumba ya biashara". Wanafunzi wake wakakumbuka ya kuwa imeandikwa: Wivu wa nyumba yako utanila. Basi Wayahudi wakajibu, wakamwambia: “Ni

ishara gani utuonyeshayo, kwamba unafanya haya?” Yesu akajibu, akawaambia: “Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha”. Basi Wayahudi wakasema: “Hekalu hili lilijengwa katika muda wa miaka arobaini na sita, nawe utalisimmisha katika siku tatu?”. Lakini yeye alinena habari za hekalu la mwili wake. Basi alipofufuka katika wafu, wanafunzi wake wakakumbuka ya kuwa alisema hivi, wakaliamini lile andiko na lile neno alilolinena Yesu.

Hata alipokuwapo Yerusalemu kwenye sikukuu wakati wa Pasaka, watu wengi waliamini jina lake, walipoziona ishara zake alizozifanya. Lakini Yesu hakujiaminisha kwao; kwa kuwa yeye aliwajua wote; na kwa sababu hakuwa na haja ya mtu ku- shuhudia habari za mwanadamu; kwa maana yeye mwenyewe alijua yaliyomo ndani ya mwanadamu.

54-56

Mt. 4: 23 (Lk. 4: 15). Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundi-
59 sha katika masinagogi yao (, akitukuzwa na watu wote.) na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu.

Mk. 1:21-28 (Lk. 4: 31-37) . Wakashika njia mpaka Kapernaumu, na 59
mara siku ya sabato akaingia katika sinagogi akafundisha. Wakashangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi.

Na mara palikuwapo ndani ya sinagogi lao mtu mwenye pepo mchafu; akapaaza sauti, akisema: “(Acha!) Tuna nini nawe, Yesu wa Nazareti? Je! umekuja kutuungamiza? Nakutambua u nani, Mtakatifu wa Mungu”. Yesu akamkemea, akisema: “Fumba kinywa, umtoke”. Yule pepo mchafu akamtia kifafa, akalia kwa sauti kuu, akamtoka (asimdhuru neno).

Wakashangaa wote, hata wakaulizana, wakisema: “Nini hii? Ni elimu mpya! Maana kwa uweza awaamuru hata pepo wachafu, nao wantii”. Habari zake zakae-
nea mara kotekote katika nchi zote kandokando ya Galilaya.

Mt. 8: 14-15 (Mk. 1: 29-31; Lk. 4: 38-39). Hata (mara walimlka katika 60
sinagogi, walifika nyumbani kwa Simoni na Andrea, pamoja na Yakobo na Yohane) Yesu alipofika nyumbani kwa Petro, akamwona mkwewe Petro, mamaye mkewe, amelala kitandani hawezi kwa homa (na mara wakamwambia habari zake).
XXIV

Akamgusa mkono, (akamwinua, akaikemea ile homa) homa ikamwacha; naye (mara hiyo) akaondoka, akawatumikia.

Mt. 8: 16-17 (Mk. 1: 32-34; Lk. 4: 46-41) . Hata kulipokuwa jioni (na jua 61
limekwisha kuchwa), wakamletea (wote waliokuwa hawawezi, na) wengi wenye pepo; (na mji wote ulikuwa umekusanyika mlangoni.) Akawatoa pepo kwa neno lake, akawaponya wote waliokuwa hawawezi, ili litimie lile neno lililonenwa na nabii Isaya, akisema: “Mwenyewe aliutwaa udhaifu wetu, na kuyachukua ma-
gonjwa yetu”. (Pepo nao waliwatoka watu wengi, wakipiga kelele na kusema: “ Wewe u Mwana wa Mungu” Akawakemea, asiwaache kunena, kwa sababu walimjua kuwa ndiye Kristu.)

Mk. 1: 35-39 (Lk. 4: 42-44) Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, 62
akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko (maku-
tano wakamtafuta-tafuta, wakafika kwake, wakataka kumzuia asiondoke kwao). Si-
moni na wenziwe wakamfuata; nao walipomwona wakamwambia: “Watu wnte wa-

nakutafuta”. Akawaambia: “Twendeni mahali pengine, mpaka vijiji vilivyo karibu, nipate kuhubiri huko nako (habari njema ya ufalme wa Mungu): maana kwa hiyo nalitokea”. Akaenda akihubiri katika masinagogi yao, katika nchi) yote ya Galilaya, na kutoa pepo.

Mk. 1: 40-45 (Lu. 5: 12.16) (Ikawa, alipokuwa katika mmojawapo wa 63
mije ile,) akaia wake mtu mwenye ukoma, akamsihi na kumpigia magoti,
na kumwambia: “Ukitaka, . waweza kunitakasa”. Nave akamurumia. akanyvasha
mkono wake, akamgusa, akamwambia: “Nataka, takaasika”. Na mara ukoma wake
ukamtoka, akatakasika. Akamkataza kwa nguvu, Akamwondoa mara, akamwambia: “Angalia,
usimwambie mtu neno lolote, ila enenda zako ukajionyeshe kwa
kuhani ukatoe alivyoamuru Musa kwa kutakasika kwako, iwe ushuhuda kwao”..
Lakini akatoka, akaanza kuhubiri maneno mengi, na kulitangaza lile neno, hata
Yesu asiweze tena kuingia mjini kwa wazi; bali aliltuwako nje mahali pasipokuwa
na watu (akaomba), wakamwendea (makutano mengi) kutoka kila mahali (wamsikilize na
kuponywa magonjwa yao).

Mt. 9: 1 (Mk.2: 1). Akapanda chomboni, akavuka, akafika mjini kwao.

64.1 Mt. 4: 18 na 21 (Mk. 1: 16 na 19; Lk. 5: 1-2). (Ikawa makutano walipomsonga
walikisikiliza neno la Mungu , yeye alikuwa amesimama kando ya ziwa la Genesareti.)
Naye alipokuwa akitembea kando ya bahari ya Galilaya, aliona ndugu wawili,
Si moni aitwaye Petro, na Andrea nduguye, wakitupa jarife baharini; kwa maana
walikuwa wavuvi.
Akaendelea mbele, akaona ndugu wengine wawili Yakobo wa Zebedayo na
Yohane nduguye, ambao walikuwamo chomboni pamoja na Zebedayo baba yao,
wakizitengeneza nyavu zao, akawita.

Mt. 9: 2-8 (Mk. 2: 2-12; Lk. 5: 17-26). (Ikasikiwa ya kwamba yumo 64
nyumbani, wakakusanyika watu wengi, isibaki nafasi hata mlangoni; akawa
akisema nao neno lake) (; na Mafarisao na waalimu wa torati walikuwa wameketi
hapo, waliotoka katika kila kijiji cha Galilaya na Uyahudi, na Yerusalemu; na uweza wa Bwana
ulikuwapo apate kuponya”.
Na tazama, wakamletea mtu mwenye kupooza, amelala kitandani (anayechukuliwa na watu wanne)
(wakataka kumpeleka ndani na kumweka mbele yake. Hata walipokosa nafasi ya kumpeleka ndani
kwa ajili ya lile kundi la watu, walipanda juu
XXV

ya dari, (waliitoboa) wakampisha katika matofali ya juu, wakamshusha yeye na kitanda chake
katikati mbele ya Yesu).

Naye Yesu, alipolona imani yao, alimwambia yule mwenye kupooza: “Jipe moyo
mkuu, mwanangu; umesamehewa dhambi zako”

Na tazama, baadhi ya waandishi (na Mafarisayo) wakasema nafsini mwao:

“(Mbona huyu anasema hivi?) Huyu anakufuru. (Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa
mmoja, ndiye Mungu?)”.

Naye Yesu hali akijua (rohoni mwake) mawazo yao, akasema: “Mbona mnawaza maovu mioyoni
mwenu? Kwa maana rahisi ni lipi, ni kumwambia (mwenye ku-
pooza): umesamehewa dhambi zako, au ni kusema: ondoka, (ujitwike kitanda
chako) uende? Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe
dhambi: (amwambia yule mwenye kupooza) ondoka, ujitwike kitanda chako, uende nyumbani
kwako”.

Akaondoka (akajitwika kitanda chake), akaenda zake nyumbani kwake (mbele
yao wote) (, akimtukuza Mungu). Makutano walipomwona, walishikwa na hofu,

wakamtukuza Mungu, aliyewapa watu amri ya namna hii (wakajaa hofu, wakasema: “Leo tumeona mambo ya ajabu”).

Lk. 5: 3-8. Akaingia katika chombo kimoja, ndicho chake Simoni, akam- 65
64.7 taka, akipeleke mbali kidogo na pwani. Akaketi, akawafundisha makutano ali chomboni. Hata alipokwisha kunena, alimwambia Simoni: “Tweka mpaka kilindini, mkashushe nyavu zenu mvue samaki”. Simoni akajibu akamwambia: “”Bwana mkubwa, tumefanya kazi ya kuchosha usiku kucha, tusipate kitu; lakini kwa neno lako nitazishusha nyavu” Basi, walipofanya hivyo walipata samaki wengi mno, nyavu zao zikaanza kukatika; wakawapungia mikono washirika wao waliokuwa katika chombo cha pili, waje kusaidia; wakaja wakavijaza vyombo vyote viwili, hata vikataka kuzama. Simoni Petro alipoona hayo, alianguka magotini pa Yesu, akisema: ”Ondoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mtu mwenye dhambi, Bwana.”

Mt. 4: 19-20 na 22 (Mk. 1: 17-18; Lk. 5: 9-11). (Maana alishikwa na ushangao, yeye na wote waliokuwa pamoja naye, kwa sababu ya wingi wa samaki walioukata.) <Yesu> akawaambia: “Nifuatani, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu” Mara <Petro na Andrea> wakaziacha nyavu zao, wakamfuata (Na kadhalika Yakobo na Yohane, wana wa Zebedayo, waliokuwa washiriki wa Simoni.) (Mara akawaita)
Nao wakaziacha chombo na baba yao, (wakaacha vyote,) wakamfuata.

66 - 78

Maria Valtorta

INJILI
KAMA NILIVYOFUNULIWA

Kuzaliwa na kutawa
kwa Maria na Yesu

1. Fikiria ya utangulizi.
Mungu alitaka uzazi usio na doa.

“Bwana alikuwa nami katika mwanzo wa njia yake”
Mithali – sura ya 8, aya 22

22 Agosti 1944. -

1.1 'Yesu ananiamuru: ”Ushike daftari mpya kabisa na kunnkili imla ya siku 16 Agosti katika ukurasa wa kwanza. Kitabu hicho kitazungumza habari za Yeye”.
Ninatii na kufuatisha.

16 Agosti 1944.

1.2 Yesu anasema:
“Leo andika hayo tu! Utakatifu ni muhimu sana. Hivyo tu mwanamke aliweza kumpokea na kumshika uzazini Yule asiyeweza kuambataniwa. Aliweza hiyo sababu alikuwa na usafi bora kabisa ambao kiumbe cha Mungu aweze kuwa nao.
Utatu Mtakatifu ulishuka kutoka Mbinguni pamoja na ukamili wake na bila kupunguzwa na

ukubwa wake bila miisho, ukakaa katika nafasi ndogo sana na kujifumbua na aina hizo:

Ni Baba Mwumbaji tena kama katika ile siku ya sita. Aliumba "Binti" mmoja wa kweli anayestahili Mungu na kumfanana. Muhuri ya Mungu imechorwa kikamilifu ndani ya Maria. Mzaliwa wa kwanza wa Baba tu amemzidi kwa ukamilifu huo. Maria anaweza kuitwa "Mzaliwa wa pili" wa Baba kwa sababu ni wa pili kufuatana na Mwana wa Baba kwa ajili ya ukamilifu uliopewa na kulindwa naye, pia kwa ajili ya heshima yake kuwa Mchumba na Mama wa Mungu; tena kwamba yu Malkia wa mbingu Yeye ni wa pili katika mawazo yake Baba kutoka umilele ambaye amependekezwa naye tangu milele yote.

Ni Mwana, aliyekuwa kwake Maria pia "Mwana", aliyemfundisha, kwa nguvu ya fumbo la neema, ukweli na hekima alipokuwa mimba bado ndani yake uzazini.

Ni Roho Mtakatifu, atakavyowatokeza watu kama katika sikukuu ya Pentekoste ambayo na sasa iliyotangulishwa, alikuwa Upendo ndani ya "Yeye aliyempendwa naye". Roho Mtakatifu
2

alikuwa tulizo la watu kwa ajili ya tunda la uzazi wake, Yesu Mtakatifu, na umama wake Maria.

3 Mungu, kwa kujitokeza kwa watu katika umbo jipya na kamili 1.3

lilioanza wakati wa Ukombozi, hakuchagua nyota ya mbinguni iwe kiti chake cha enzi wala nyumba ya mtawala mkuu. Vile vile hakuchukua mabawa ya malaika yawe kiti cha kuegemea miguu yake, mbali, alitaka uzazi usio na doa.

Hawa pia aliumbwa bila doa, na alizingiriwa na ulimwengu wenye hali bado safi. Lakini yeye kwa hiari yake alitaka kujiharibu. Bali Maria aliyeishi katika dunia iliyozorota hakutaka kupunguza usafi wake hata kwa wazo moja la dhambi. Alifahamu kwamba dhambi zipo. Aliziona jinsi zilivyo na nyuso nyingi na mbaya sana. Aliziona zote. Hata ile mbaya kabisa: mauaji ya Mungu. Lakini alifundishwa kuzijua dhambi ili aweze kufidia na ili awe Yeye Mwenye huruma na kuwaombea wakosaji uokovu.

4 Fikira hiyo ni utangulizi wa mambo matakatifu mengi ni- 1.4
takayokufunulia wewe na kwa watu wengi kuwa tulizo lenu".

2. Yoakine na Ana wanamwekea Mungu nadhiri moja.

22 Agosti 1944.

1 Naona ndani ya nyumba moja. Mwanamke mzee anaketi karibu 2.1

na kitanda cha mfumi. Nakisia, nikitazama unywele uliokuwa zamani mweusi bila shaka na sasa huwa mweupe, na nikiona uso wake bila vifinyo lakini wa namna fikira na heshima kutokana na miaka mingi, kwamba anaweza kuwa na miaka hamsini au hamsini na tano.

Nikikadiria umri huo wa mwanamke naegamia uso wa mama yangu. Ninatambua sura yake vizuri siku hizi ninapokumbuka siku zake za mwisho kandoni pa kitanda changu... Kesho kutwa itakuwa mwaka mzima tangu alipofariki dunia... Uso wa mama yangu ulikuwa wa kijana ingawa nywele zilikuwa nyeupe mapema mno. Alipotimiza miaka hamsini alikuwa na nywele nyeupe na nyeusi kama hapo mwishoni mwa maisha yake. Lakini, isipokuwa na uzito wa tazamo lake, hakuna kitu kilichoonyesha umri wake. Kwa hiyo ningaliweza kudanganyika katika kisio la umri wa mwanamke mzee.

Huyo ninamwona akifuma, ndani ya chumba chenye uangavu sana kutoka mlangoni. Palipofunulika mtazamo unakwenda bustanini ambapo uelekeo ni kubwa kama kiunga kwa sababu inatandaa ikipanda na kutelemka na shamba la nyasi chanikiwiti. Mwanamke

3

ana ubora aklwa wajiji ya Mwebrania wa kweli. Macho yake meusi na marefu yanankumbusha, sijui kwa nini, yale macho ya Yohane Mbatizaji. Ni macho yenye fahari kama la malkia lakini pia la upendo. Ni kama kwamba kimeto chake cha tai kingefunikwa na tandabui la samawi. Macho ya upole, na yenye huzuni kidogo, kama ya mtu anayewaza mambo yaliyopita. Rangi ya uso ni

kahawia lakini si sana. Kinywa chake, kipana kidogo, kimechorwa vizuri na kinabaki kwa nguvu bila ukali. Pua yake ni ndefu tena nyembamba, inapindika kama mdomo wa tai na inakubalika na macho hayo. Umbo lake si nene, linganifu, pengine ni mrefu nikikadiria jinsi anavyoketi.

Nahisi kwamba anafuma ukingo au zulia. Ngalawa zenye rangi mbalimbali zinakwenda na kurudi upesi juu ya mshindio mwenye rangi ya ngeu. Kazi iliyomalizika huonyesha msuko mzuri wa mapambo yenye rangi za kijani kibichi, za kimanjano, nyekundu na buluu kali zinazopitana na zinazoyeyuka kama kwenye sanamu iliyofanyika kwa kupanga vigae vyenye rangi mbalimbali. Mwanamke huyo anavaa nguo ya mfuto yenye rangi ya urujuani, inayofanana na maua ya rangi ile ile.

2 Amasimama anaposikia kubishwa mlangoni. Ni mrefu kweli! Anafungua 2.2 mlango.

Mwanamke mwingine anamwuliza: “Ana, wataka kunipa mtungi? Nitaujaza kwa ajili yako”.

Mwanamke huyo anasindikizwa na mvulana, wa miaka mitano, anayeshika mara nguo ya Ana anayembembeleza anapoingia katika chumba kingine na kurudi na mtungi mzuri wa shaba anautolea mwanamke huyo akisema: “U mwema daima kwa Ana mzee, Mungu akurudishie kwa mwana huyo na wana wako walio hai na watakaokuja bado, wewe mwenye bahati!”. Ana anasikitika.

Mwanamke anamtazama na hajui la kusema kwa sikitiko lake. Kwa kumtuliza na kubadilisha mawazo, anasema: “Nakuachia Alfayo, hapo kama hakusumbui, hivyo nitakwenda upesi zaidi, na ninaweza kukujazia mitungi mingi na mabalasi mengi”. Alfayo anafurahi kubnki na inaeleweka kwa sababu gani. Mara mama yake alipoondoka Ana anamwinua, na kumchukua bustani. Anambeba na kumpeleka kwenye mizabibu yenye rangi ya kitani kama topazi, akasema: “Ule, ule, ni tamu”, akimbusu usoni penye mchuzi ya matunda yanayokonyolewa na mtoto kwa furaha. Baadaye anacheka kwa moyo, akionekana mara kijana zaidi, kwa meno yake mazuri yanayojionyesha, na kwa furaha usoni, mtoto anaposema: “Na sasa unanipa nini?” akimtazama kwa macho yake makubwa yanayokazwa, yenye rangi ya kijivu nili. Anacheka na kucheza akikunja magoti akisema: “Unanipa nini nikikupa....nikiku-

4

pa...kisia!”. Na mtoto apiga makofi, akicheka kabisa: “Busu, busu nakupa. Ana mzuri, Ana mwema, Ana mama!”.

Ana, akisikia anaitwa: “Ana mama”, anatoa sauti pendevu la furaha akamkumbatia mtoto, akisema: “Loo! Mpenzi! Mpenzi! Mpenzi!”. Kwa kila “mpenzi” busu moja laanguka katika mashavu mekundu ya uso wake. Halafu waelekea kabatini, na kwenye sahani atoa vinyunya vyenye asali. “Nilikupikia, muhebi wa Ana maskini, kwako unipendaye. Uniambie, wanipenda kiasi gani?”. Na mtoto akifikiria kitu kilichomshtusha zaidi anasema: “Kama Hekalu la Bwana”. Ana anambusu tena kwenye macho machangamfu, kwenye kinywa chekundu, na mtoto anajisugua juu yake kama kipaka.

Mama aenda na kurudi na mtungi uliojazwa, akicheka bila kusema. Awaacha katika ukunjufu wao wa moyo.

3 Mtu mzee anaingia bustanini. Ni mfupi kidogo kuliko Ana, ki- 2.3

chwa chake chenye vunga la nywele za mvi wote. Uso wake mwangavu na ndevu zilizoubwa mraba, macho ya samawi nyeupe katikati ya vipaji vya rangi ya hudhurungi inayoelekea rangi ya shaba. Anavaa nguo yenye rangi ya ngeu.

Ana hamwoni kwa sababu mlango uko nyuma yake, naye anamsongea akisema: “Na kwangu mimi hakuna kitu?”. Ana anageuka akasema: “Ee Yoakine, umemaliza kazi yako?”. Wakati ule ule mtoto Alfayo anamkimbilia magotini, akisema: “Hata kwako kwako”. Na mzee anapoinama akambusu, mtoto anajitupa shlngoni mwake akimchafua ndevu kwa mikono na busu.

Yoakine naye ana kipaji chake: anaweka mkono wa kushoto mgongoni akitoa pera zuri sana linalofanana na chombo cha kaure, akacheka akimwambia mtoto anayenyosha mikono kwa hamu: “Ngoja nikukatiekatie. Huwezi namna hii. Ni kubwa zaidi kuliko wewe”, na kwa kisu kifupi,

aliye nacho kiunoni, kisu cha kupogolea, anakata vipande vipande vya pera, na inaonekana kama anatia chakula katika kinywa cha faranga, jinsi anavyotia kwa taratibu mamego ya chakula ndani ya kile kinywa kidogo wazi, kinachotafunatafuna.

“Tazama macho yale ajabu, Yoakine! Hayafanani na vipande viwili vya ziwa la Galilaya, upepo wa jioni unaposukuma utando wa wingu mbinguni?”. Ana anasema akitegemea mkono wake begani kwa mumewe na kujiegemeza kwake kidogo, konyezo linaloonekana upendo mkubwa wa mke, upendo usioharibika baada ya miaka mingi ya unyumba.

Na Yoakine anamkazia macho kwa upendo akiridhia akisema: “Mazuri sana! Na misokoto ya nywele! Haina rangi ya nafaka iliyokauka juani? Tazama, na ndani yake rangi ya dhahabu na sha-

5

ba zimechanganyika”.

2.4 4 “Laiti tungalikuwa na mtoto ningalimpenda hivyo, na macho haya na nywele hizi...”. Ana ameinama, hadi amepiga magoti, na kuyabusu macho yake makubwa mawili yenye rangi ya buluu-kijivu akisilitika sana.

Yoakine naye anasikitika. Lakini anataka kumfariji. Anamwekea mkono wake juu ya nywele zake za kipilipili na mvi na kusema: “Lazima kutumaini zaidi. Mungu anaweza mambo yote. Mpaka twaishi mwujiza waweza kutokea, mradi tumpende Yeye na kupendana kati yetu”. Yoakine anakaza sana maneno ya mwisho.

Lakini Ana ananyamaza, akisikitika, anakaa kichwa kilichoinama kwa kutoonyesha machozi mawili yanayoshuka na yanayogunduliwa na mtoto Alfayo tu. Huyo akiwa na nyongeza ya huzuni kwa sababu rafiki yake mkuu analia machozi kama yeye mwenyewe pengine, ananyosha kimkono chake na kufuta machozi yale.

“Usilie machozi Ana! Twafurahi mamoja. Mimi walau, ninafurahi kwa sababu nina wewe”.

“Nami kwa ajili yako, lakini sikukupa mwana... Nahisi kwamba sikumpendeza Bwana, ili anifanye tasa...”.

“Ee mke wangu! Kwa nini ungalimchukiza, wewe, mtakatifu ?

Usikilize. Twende mara moja tena, Hekaluni kwa nia hiyo. Siyo kwa sikukuu ya Vibanda tu. Tufanye sala ndefu. Labda utatendewa kama Sara... jinsi ya Hana mke wa Elkana. Walingoja muda mrefu na kuogopa kuwa wapotevu sababu hawakuwa na mtoto. Bali kwa wakati huu mbinguni, kwa Mungu, mwana mtakatifu alitayarishwa. Ufurahi Bimkubwa wangu. Kilio chako kinaniumiza zaidi kuliko kasoro ya kutokuzaa mtoto... Tutamchukua Alfayo pamoja nasi. Tutamwombesha yeye asiye na hatia... na Mungu atapokea sala yake na yetu pamoja na kuzisikiliza”.

“Ndiyo, tuweke nadhiri kwa Bwana. Mzaliwa awe mali yake. Mradi atujalie... Ee! Kusikia kuitwa “mama “! “.

Na Alfayo, anayetazama akishangaa kwa uadilifu anasema: <<Mimi nakuita”.

“Ndiyo mpenzi wangu... lakini... wewe mama unaye, nami... mimi mtoto sinaye...”.

Ono langu hapa limekwisha.

2.5 5 Nafahamu kwamba kipindi cha muda wa Bikira Maria kuzaliwa kimeanza. Na ninafurahi sana kwa sababu nilikitazama kwa hamu. Nadhani kwamba nawe pia utakifurahia.

Kabla sijaanza kuandika, nimesikia Mama akiniambia: “Binti basi, andika juu yangu. Utafarijiwa katika dhiki zako zote”. Na wakati aliposema hilo, aliniwekea mkono wake kichwani kwa bem-

6

belezo tamu. Halafu ono limekuja. Lakini mwanzoni, kabla sikuwa nimesikia jina la huyu mwanamke mwenye miaka hamsini, sikutambua kwamba nilikuwa mbele ya mzazi wake Mama Maria na ndiyo mbele ya jalio la kuzaliwa kwake.

3. Sikukuu ya Vibanda.
Yoakine na Ana walikuwa na Hekima.

23 Agosti 1944.

1 Kabla ya kuendelea naandika maelezo. 3.1

Nyumba haikuonekana kadiri yangu kama ile ya Nazareti najuayo sana. Hasa mazingira ni tofauti sana. Hata bustani ni pana zaidi, na mbele yaonekana mashamba. Si mengi, lakini basi kuna. Baadaye, Maria akiisha kuolewa, niliona bustani tu pana zaidi, lakini halikuwako eneo lote la mazao mengine ila bustani ya miboga tu. Pia chumba ninachokiona ni tofauti na vyumba nilivyoviona katika maono mengine. Nahisi kuwa labda wazazi wa Maria, kwa ukosefu wa fedha, waliuza sehemu ya mali zao. Au pia, baada ya Maria kurudi kutoka Hekaluni, alienda kuishi katika nyumba nyingine.

Huenda aliipewa na Yosefu. Sikumbuki kama maono na mafundisho yaliyopita yangalinithibitisha kwamba nyumba ya Maria kuzaliwa ni pia nyumba ile ile ya Nazareti.

Nimechoka sana. Na ninasahau mara maneno ninayoambiwa hasa kwa imla. Lakini amri zake na nuru inaendelea rohoni mwangu ukumbusho. Lakini jambo moja moja latoweka mara. Ikiwa baada ya saa moja ningepata kusema tena niliyosikia, singejua kitu zaidi, ila maneno machache ya maana. Bali maono yanabaki hai sa-
babu nimeshurutishwa kuyatazama mimi mwenyewe. Imla nazipokea. Maono yale bali ni juu yangu kuyafahamu. Hivyo yanakaa hai katika akili yangu iliyojitahidi kuyakumbuka katika matukio yao.

Nalitumaini ya kupokea imla juu ya ono lajana. Bali haiko.

2 Naanza kuona na kuandika. 3.2

Nje ya maboma ya Yerusalemu, juu ya milima na katikati ya mizeituni, kuna umati wa watu. Yaonekana kama soko kubwa sana. Lakini meza na vibanda haziko. Sauti ya vishindo na milio ya walimi na wauzaji hazisikiliki. Michezo haiko. Kuna hema nyingi za sufi ya mfuto, kweli zisizovuja maji, zilizotandwa juu ya vyango vilivyokitwa. Na vyango vimefungwa matawi yenye majani mabichi kwa ajili ya kupamba na kuburudisha. Hema nyingine, bali zimefumwa na matawi yaliyokitwa na kufungwa hivyo ^ na kuumba

7

namna ya vijia vidogo vya majani mabichi. Chini ya kila hema watu wa kila umri na cheo wanazungumza kwa upole na utulivu, na mazungumzo haya yakatwa pengine na vifijo vya watoto tu.

Kunakuchwa, na nuru za taa za mafuta zinan'gaa huko na huko katika kambi isiyo ya kawaida. Kandokando ya mianga jamaa nyingine wanakula chakula cha jioni wakikaa chini. Akina mama wanapakata watoto wadogo, miongoni mwao wengi wamechoka na kulala usingizi. Wanashika bado kipande cha mkate katika vidole vyao vidogo vyenye rangi ya waridi. Wanaviegemeza vichwa vyao kwenye vifua vya mama zao kama vifaranga chini ya kuku. Akina mama wanamaliza mlo wawezavyo, kwa mkono mmoja tu mwenye nafasi, mwingine ukumbatia mtoto. Jamaa nyingine, bali, hawajaanza kula, wanazungumza katika utusitusi wa ukungu wa jioni, wakingoja chakula kinachotayarishwa. Mioto inawaka huko na huko na kandokando wanawake wanashughulika. Matumbuizo mengine polepole, ningesema mithali ya malalamiko, yamtuliza na kumfilitisha mtoto mchanga usingizi.

Angani juu uangavu unazidi kuwa buluu kali hata kuonekana pazia kubwa kabisa la mahameli nyororo yenye rangi ya nyeusi-buluu, ambapo wasanaa na wapakaji wanapoweka polepole vito na vibatari, vingine vya pekee, vingine vilivyofanya mistari ya elimu, umbo la ajabu. Kati ya hizo nyota ziko hasa Dubu kubwa na ndogo zinazotangulia na umbo lake la gari lenye mlingoti ulioegamia chini, baada ya kufungua ng'ombe kutoka kongwa. Nyota ya kaskazini inachekeka na kumetameta sana.

Nafahamu kwamba ni Oktoba kwa sabatu mtu mmoja anasema kwa sauti nzito: "Oktoba hiyo nzuri kama chache zilikuwako!"

1.3 3 Tazama, Ana anakuja kutoka penye moto mmoja na vitu mikononi, vilivyotandikwa juu ya mkate mpana na sawa kama kinyunya na hutumika kama sinia. Alfayo anamshikia marinda na kunenanana kwa sauti yake ndogo. Yoakine, mtilizini pa kibanda chake kidogo cha matawi, anazungumza na mtu mwenye umri wa miaka karibu na thelathini - anayesalimiwa kutoka mbali na Alfayo kwa sauti akisema: “Baba” - na anapoonana Ana akisogea anafanya hima kuwasha taa ndogo.

Ana anapita akienda kwa makini katikati ya mitaa ya vibanda. Makini na mnyenyekevu. Hana maringo na mtu ye yote. Anainua mtoto wa mwanamke mmoja maskini, maskini sana, aliyekuwa ameanguka miguuni pake, na, kwa kuwa amechafuka uso kwa ardhi na kulia machozi, anamsafisha na kutuliza, akimrudishia mama yake, anayemkimbia na kumwomba radhi, akisema: “Ee! Si kitu! Nafurahi kwamba hakujiiumiza. Ni mtoto mzuri. Umri wake, je?”

8

“Miaka mitatu. Ni wa mwisho ila mmoja, na karibuni nitapata mwingine. Nina watoto sita wa kiume. Ningependa kuwa na mtoto wa kike sasa... Kwa mama, kuwa na mtoto wa kike, ni muhimu sana...”

“Yeye Aliye juu alikufariji sana mama” Ana anasikitika.

Na yule mama: “Ndiyo. Mimi maskini, lakini wana ni furaha yetu na walio wakubwa zaidi wameanza kusaidia kazini. Nawe, bibi (lote laonyesha kwamba Ana ni wa cheo bora zaidi, na mwanamke anaona) una watoto wangapi? “.

“Sinao.”

“Hakuna? ! Na huyo si wako? “.

“Sio, ni wa jirani mwema sana. Ni tulizo langu...”.

“Walikufa, ila...”.

“Sikuwapata kabisa”.

“Lo!” Mwanamke maskini anamtazama kwa huruma.

Ana anamwaga kwa sikitiko na kuelekea kibanda chake.

“Nimechelewa, Yoakine. Amenichelewesha mwanamke maskini, mama mwenye wana sita wa kiume, fikiri! Na karibu atampata mwana mwingine”.

Yoakine anasikitika.

Baba ya Alfayo anamwita mtoto wake, lakini huyo anasema: “Mimi nakaa na Ana. Namasaidia” Wote wanacheka.

“Mwache. Hasumbui. Halazimishwi kwa sheria bado. Hapa au pale ni kama kidege alaye tu” Ana kisha sema haya anapakata mtoto na kumpa kinyunya na tonge, labda la samaki iliyokaangwa. Naona kwamba anaitengeneza kabla ya kumpa. Labda anaondoa miiba. Kwanza amepakulia mumewe chakula. Mwishowe anakula yeye mwenyewe.

4 Nyota zinakithiri katika usiku na taa zinakithiri pia katika 3.4 kambi. Baadaye, pole pole taa nyingi zinazimika. Ni za wale waliokula chakula kwanza na sasa wanalala. Na sauti zinanyamaa pole pole. Sauti za watoto hazisikizwi tena. Watoto wachanga wengine tu wanalia kama kondoo anayetafuta maziwa ya mama. Upepo mwanana wa usiku unavuma juu ya vitu na binadamu, na kufutia mbali maumivu na makumbuko, matumaini na vinyongo. Lakini matumaini na vinyongo zadumu, ingawa yamepunguka, katika usingizi, katika ndoto.

A na anasema na mumewe, akimpakata Alfayo anayepata usingizi mikononi mwake: “Usiku huu nimeota kwamba mwaka ujao nitakuia Mji Mtakatifu kwa sikukuu mbili badala ya moja tu. Na sikukuu moja itakuwa sadaka Hekaluni ya kiumbe changu...! Yoakine...!”

9

“Tumaini, tumaini, Ana. Hukusikia neno jingine? Bwana hakunon'gona neno moyoni mwako? >>.

“La, ndoto tu...”.

“Kesho itakuwa siku ya mwisho ya sala. Sadaka zote zimekwisha tolewa. Lakini tutazitoa kesho tena, kwa heshima ya hadhara. Tutampendeza Mungu kwa upendo wetu mwaminifu. Nafikiri

daima kwamba litakutokea jinsi ya Hana mke wa Elkana”.

“Mungu anijalie... laiti angekuwepo mwenye kuniambia mara: 'Nenda kwa amani. Mungu wa Israeli amekujalia neema uliyoiomba!' “.

“Neema ikija, kitoto kichanga atakuambia akiruka mara ya kwanza kwa furaha tumboni mwako, na itakuwa sauti ya malaika, kwa hiyo sauti ya Mungu”.

Sasa kambi inatulia katika giza. Ana pia anamrudisha Alfayo katika kibanda jirani na kumlaza juu ya malalo ya nyasi kavu kandokando ya nduguze walioanza kulala usingizi. Baadaye anakwenda kulala karibu na Yoakine, na taa yao pia, mojawapo kati ya nyota za mwisho duniani, inazimika. Nyota nzuri zaidi mbinguni zinakaa na kuwakeshea wanaosinzia.

3.5 Yesu anasema:

“Wenye haki ni daima wenye akili kwa sababu wakiwa rafiki wa Mungu, huishi pamoja naye anayewafundisha; Yeye Aliye Hekima isiyo na mipaka.

Babu wangu na Bibi walikuwa na haki, kwa hii walikuwa na hekima. Waliweza kusema kweli ilivyo katika Kitabu, kinachosifu Hekima: “Niliipenda tangu ujana wangu na kuitafuta-tafuta, nikitamani kujichukulia hiyo mithili ya bibi arusi”.

Hana wa Haruni alikuwa mke mwema, jinsi anavyosema Babu yenu. Na Yoakine, wa ukoo wa mfalme Daudi, hakutafuta uzuri wala utajiri, bali alitafuta utakatifu. Ana alikuwa na wema mkuu. Fadhila zote ziliunganisha pamoja kwake kama shada la maua yenye manukato, kwa kuwa jambo zuri sana la pekee: ule Wema, Wema wa kifalme kwa kuweza kusimama mbele za Mungu.

Yoakine basi amejifunga na hekima mara mbili “akimpenda zaidi ya mwanamke mwingine ye yote”: na kuioa hekima ya Mungu iliyofungwa katika moyo wa mke mwenye haki. Hana wa Haruni hakutafuta kitu isipokuwa kuunga maisha yake na yale ya mtu mwenye

3.6 haki, akiamini kwamba furaha ya jamaa ni uadilifu. 6 Kwa kuwa mfano wa 'mwanamke bora' alikosa taji ya wana tu, sifa na haki za

mwanamke aliyeolewa, anavyosema Sulemani. Watoto hawa tu bado walikosekana kujaza furaha. Wangukuwa kama maua ya mti

10

uliokuwa kitu kimoja na mti ulio karibu, na kuzaa matunda mapya mengi, mnamo ladha mbili zinaungana kuwa moja. Ana, kwa upande wa mumewe, alikuwa hajapata kabisa ghairi yo yote mpaka sasa.

7 Yeye alikuwa akizeeka. Mke wa Yoakine tangu miaka mingi sa- 3.7 na, daima alikuwa kwa mumewe “bibi arusi wa ujana wake, furaha yake, ayala apendaye na paa apendzaye”. Upendo wake ulikuwa umeendelea kuburudisha daima kama mshangao wa usiku wa kwanza wa arusi na ulikuwa umevuta kwa utamu moyo wake akiulinda kipya kama ua linalorutubishwa na umande, na akiuchoma kama moto, ambao mkono huamsha siku zote. Kwa hii katika uchungu wao wa kutokuwa na wana, walikuwa wakisema wao kwa wao “maneno ya faraja wakati wa masumbuko na taabu”.

8 Na Hekima ya milele, wakati ulipowadia, baada ya kuwafundi- 3.8 sha ulimwenguni iliwaangaza katika ndoto za usiku, nyota ya utenzi wa utukufu iliyopaswa kuja kwa ajili yao, ndiye Maria Mtakatifu sana, Mama yangu. Hawafukiri hayo kwa unyenyekevu wao lakini moyoni mvao walitetemeka kwa tunaini wakati wa mlilo wa kwanza wa ahadi ya Mungu. Kweli ni hakika katika maneno ya Yoakine 'Tumaini tumaini... Tutampendeza Mungu kwa upendo wetu mwaminifu'. Walimtamani mwana: walimpata Mama wa Mungu.

9 Maneno ya kitabu cha Hekima yaonekana yameandikwa kwa ku- 3.9 sudi lao: “Kwa ajili yake nitatukuzwa katika makutano... Kwa ajili yake nitajaliwa kupata sifa ya milele, na kuwaachia wanifuatao kumbukumbu la daima”. Lakini kwa kupata yote haya, walipaswa umiliki wema wa ukweli na thabiti ambao tukio lo lote haliharibu. Wema wa imani. Wema wa tumaini. Wema wa upendo. Wema wa usafi wa moyo. Usafi wa bwana na bibi arusi! Wao walikuwa nao, kwa sababu si lazima kuwa na ubikira kwa kuwa na usafi wa moyo. Na malalo ya arusi yaliyo safi hulindwa na malaika, na wana wema hushuka, wanaotumia wema wa wazazi kama

kanuni ya maisha yao.

10 Lakini sasa wako wapi? Sasa wana hawatakiwi, na usafi wa 3.10 moyo pia haupendwi. Kwa sababu hii mimi nasema kwamba upendo na malalo ya arusi yametiwa unajisi.”.

4 . Ana anatangaza umama wake kwa zaburi.
Mwilini mwake ni moyo wa Maria usio na dhambi

24 Agosti 1944.

1 Ninaona tena nyumba ya Yoakine na Ana. Hakikubadilika nda- 4.1
ni, ila kwa matawi mengi yenye maua, yaliyowekwa katika gudulia
11

huku na huku, tokeo la kweli la kazi ya kupogea miti ya bustani iliyotoa maua mengi; kama wingu wenye rangi toka weupe wa theluji mpaka wekundu wa marijani fulani.

Pia kazi ya Ana ni ya aina nyingine sasa. Katika mtambo mdogo kuliko ule wa kawaida, yeye anafuma vitambaa safi vya kitani. Naye anaimba, akiogoza mwendo kwa kupiga mguu. Anaimba na kutabasamu... kwa nani? Anajiambia na kujifurahia na pia hayo anakifanyia kiumbe kilicho ndani yake.

Tenzi si ya mwendo wa haraka lakini ina uchangamfu – tenzi hiyo nimeandika hapa kando ili kuirudia, kwa kuwa yeye mwenyewe anairudiarudia akiuonja utamu wake. Pia anaitamka akikuza sauti zaidi na zaidi na kwa imara, kwa jinsi afanyavyo mtu ambaye ameukuta wimbo unaoandamana na tamaa za moyo wake, ambaye kwanza ni kama anadodosa na baadaye anaudaka kwa uthabiti - naiandika hapa tenzi hiyo nyofu lakini tamu:

“Utukufu kwa Mwenyezi Mungu aliyewapenda wana wa Daudi. Utukufu kwa Mungu!

Neema bora yake kutoka Mbinguni ilinijia.

Mti mzee umezaa tawi jipya, nami heri.

Kwa sikukuu ya Numz tumaini lilitawanya mbegu;

manukato ya Nisam sasa yaiona ikichipua.

Kama mlozi mwili wangu unatapanya maua wakati wa masika.

Tunda lake, wakati wa jioni, unaona kulichukua.

katika tawi lile ipo waridi, lipo tunda tamu sana.

Ipo nyota nyangavu, yupo malaika mtoto.

ipo furaha ya nyumba, ya bwana na bibi arusi.

Sifa kwa Mungu, kwa Bwana yangu, aliyenihurumia.

Nuru yake aliniambia: “Nyota itakujilia”.

Utukufu, utukufu! Lako litakuwa tunda hili la mti,

la kwanza na la kipeo, takatifu na safi kama tuzo la Bwana.

Lako litakuwa na kwa ajili yake furaha na amani yote ije duniani.

Ruka, ee pia. Nyuzi ishike kwa kitani cha malaika mtoto.

Yeye anazaliwa! Kwa Mungu uende wimbo wa sifa wa moyo wangu”.

4.2 2 Ana anapotaka kusema kwa mara ya nne wimbo wake Yoakine anaingia. “Umeona furaha Ana? Unaonekana kama ndege aliyeimba akitangaza wakati wa kutoa maua. Wimbo huo ni wimbo gani? Sijausikia bado kwa mtu. Unatoka wapi?”.

“Kutoka moyo wangu, Yoakine”. Ana ameinuka na sasa anaelekea mumewe, akitabasamu, mchangamfu. Anaonekana kijana na mzuri zaidi.

12

“Sikuelewa kama u mshairi” asema mumewe, akimtazama kwa mshangao wazi. Hawaonekani tena kuwa wenye ndoa wazee. Katika kuangaliana kwao kuna utamu wa upendo kama ule wa vijana waliooana sasa hivi. “Nimekuja kutoka mwisho wa bustani nikikusikia unaimba. Ilikuwa miaka mingi sikukusikia ukiimba kama hua mpendevu. Uniimbie tena wimbo huu!”.

“Ningekuimbia tena hata kama wamekabidhia wimbo daima vilio kweli kweli vya matumaini yao, na furaha, na huzuni. Mimi nimekabidhia wimbo mtindo wa kujisemea mimi na kukuelezea wewe furaha kuu. Ndiyo, kwa kujisemea mimi, kwa kuwa ni jambo kubwa kiasi ambacho, ijapo naona uhakika kabisa, nashindwa kujihakiki...” akaanza tena wimbo wake lakini, alipotaka kuendelea “katika tawi lile ipo waridi, lipo tunda tamu sana. Ipo nyota...” sauti yake nene nzuri linganifu inagwaya kwanza, na mara kukatika, na kwa kwikwi ya furaha anamkasia macho Yoakine, anainua mikono juu, na kupaaza sauti: “Mimi ni mama, wee mpenzi wangu!” akamkimbilia kifuani katikati ya mikono aliyenyosha akaifunika sasa kuzungukia bibi arusi yake mchangamfu. Kumbatio takatifu na kunjufu zaidi kuliko yote niliyoona tangu nimezaliwa. Takatifu tena la bidii nyingi katika utufu wake.

Akamlaumu Ana kwa upendo akisema, katikati ya nywele za mvi zake: “Kwa nini hukuniambia?”.

“Kwa sababu nalitaka kuwa na uhakika. Mzee kama niliye... kufahamu kuwa mama... sikuweza kusadiki ni kweli... na sikutaka kukutia ghairi nzito kuliko zote. Tangu mwisho wa Desemba najisikia kama nina kitu kipya tumboni mwangu na kuliweka, nasemavyo, tawi jipya. Lalkini sasa katika tawi hilo tunda ni yamkini... Uone? Nguo ile ya kitani ndiyo ni kwa yule anayekuja”.

“Siyo kitani ulichonunua huko Yerusalemu mwezi wa Oktoba?”.

“Ndiyo, halafu nalikifuma nilipokuwa nikingoja... na nikitumaini.

3 Nalitumaini kwa sababu siku ya mwisho, nilipokuwa nikisali 4.3
Hekaluni zaidi ya mwanamke kuruhusiwa pa Nyumba ya Mungu na jua limekuwa magharibi... ukumbuke nalisema: “Bado, bado kidogo”. Sikuweza kujitenga kutoka pale hadi nipate neema! Basi, kati ya uvuli uliokuwa ukiongezeka jioni katika mahali patakatifu, nikipoangalia kwa hamu yote ya roho yangu ili nikubaliwe mbele za Mungu aliyemo, basi nikaona cheche ya nuru ya ajabu, bora.. Mwanga mweupe kama mbalamwezi mwenye ung'arisho wa lulu na vito vyenye kumetameta duniani. Ni kama nyota za vito za Pazia au mojawapo ya nyota zilizomo miguuni pa makerubi, ambayo imekuja mbele na kung'aa kwa nuru isiyo ya ulimwengu huu... ilikuwa kama

13

inatoka katika nyuma ya Pazia takatifu, yaani kutoka Utukufu mwenyewe, moto huu ulikuwa ukinjia kwa kasi, na katika kujipatia njia angani ulitoa sauti ya wimbo wa kimbinguni: “Ulichokiomba kikujie”. Maana ndiyo ya wimbo wangu “Nyota moja itakujia”. Mwana wetu atakuwaje, ambaye anaanza kujidhihirisha kama nuru ya nyota katika Hekalu na kusema pia: “Mimi nimo” mnamo sikukuu ya Nuru? Je! umeona kwa haki ukinifikiri kama Hana mke wa 4.4 Elkana mpya?. 4 Tutamwitaje kiumbe chetu ninayesikia kuninon'gona tumboni, mpole kama wimbo wa maji kwa moyo wake mdogo, unaopigapiga kama ule wa hua mdogo aliyeshikwa katika kitanga cha mikono?”

“Akiwa wa kiume, tutamwita Samweli. Akiwa wa kike, Nyota. Neno lililosimamisha wimbo wako kwa kunipa furaha ya kujiona baba. Umbo aliopokea kwa kujitokeza katika giza takatifu ya Hekalu”

“Nyota, nyota yetu, kwa sababu huenda, nadhani ni mtoto wa kike. Naona, kwamba mabembelezo ya upendo ya namna hii, yaweza kuja kutoka mwana wa kike mpole sana tu. Kwa sababu simchukui, sioni uchungu. Yeye ndiye anayenichukua mimi katika kija cha samawi na chenye maua, kama kwamba ningechukuliwa na malaika watakatifu, na dunia imekwisha kuwa mbali... Daima nilikuwa nimewasikia wanawake kusema kwamba kuwa na mimba na kuja mzito ni uchungu. Lakini mimi sina uchungu. Najiona na nguvu, kijana na mwenye afya zaidi ya wakati

nilipokujalia ubikira wangu zamani za ujana wangu. Binti Mungu - kwa sababu ni wa Mungu zaidi kuliko wa kwetu huyo anayezaliwa kutoka shina lililokauka - hamwumizi mama yake. Bali anampeleka amani na baraka: matunda ya Mungu Baba yake ya kweli”.

“Basi tutamwita Maria. Nyota ya bahari yetu, lulu, furaha. Jina la mke mkuu wa kwanza wa Israeli. Lakini huyo hatakosa kabisa dhidi ya Bwana, na Kwake tu atampa wimbo wake kwa sababu kwake Yeye ametolewa, hostia kabla ya kuzaliwa”.

“Kwake anatolewa, ndiyo. Awe wa kiume ama wa kike, baada ya kujifurahisha miaka mitatu na kiumbe chetu tutamtotea Bwana. Hostia sisi pia pamoja nayer kwa utukufu wa Mungu”. Sioni, wala sisikii neno jmgine.

4.5 Yesu anasema:

“Hekima; akiwa aliwaangaza kwa ndoto za usiku, alishuka, Yeye, “pumzi ya uweza wa Mungu, miminiko nakawa la utukufu wake Mwenyezi”, akawa Neno kwa aliye tasa. Aliyeona sasa kwamba muda wake wa kuokoa umewadia, Mimi, Kristu, mjukuu wa

14

Ana miaka hamsini baadaye karibu kwa njia ya Neno, nitatenda miujiza juu ya tasa na wagonjwa, juu ya walio na pepo, juu ya wenye huzuni, juu ya umaskini wote wa ulimwengu.

Na, sasa hivi, kwa furaha ya kuwa na mama ninanon'gona Neno la fumbo, katikati ya uvuli Hekaluni palipowekwa matumaini ya Israeli. Hekalu hilo linafika karibu na mwisho wake. Hekalu jipya na la kweli, lisilo tena tumaini la taifa, bali thibitisho la Mbingu kwa ajili ya watu wa ulimwengu wote, hata milele na milele, hadi mwisho wa ulimwengu, linataka kutokeza duniani. Neno hilo lilitenda mwujiza wa kumpasha mimba kwa Yeye asiyeweza kuzaa, likanipa Mama, asiye na tabia bora tu, kama ingekuwa kawaida yaani akizaliwa kutoka watakatifu wawili. Na hakuwa na moyo mwema tu kama wengi wanao bado, hakuwa na mwongezo wa siku zote wa wema huo kwa bidii yake tu, hakuwa na mwili usio na dhambi ya asili tu, alikuwa wa pekee katika viumbe vyote, na roho liyo na dhambi ya asili.

6 Wewe umeuona uzazi wa kuendelea wa nafsi kutoka Mungu. Sa- 4.6
sa ufikiri ulikuwa wa namna gani uzuri wa nafsi hii iliyotazamwa kwa upendo na Baba tangu kabla nyakati hazijakuwako. Roho hii ilikuwa furaha ya Utatu Mtakatifu aliyetamani kumpamba kwa zawadi zake kwa kujitunukia Yeye Mwenyewe. Ee Mtakatifu Bora, uliyeumbwa na Mungu kwa ajili yake Mwenyewe na halafu kwa uzima wa watu. Mleta Mwokozi, wewe ndiwe ulikuwa wokovu wa kwanza. Mbingu hai, kwa njia ya kicheko chako umeanza kuitakasa dunia.

Roho iliyoubwa kwa kuwa roho ya Mama wa Mungu! Wakati, kutoka tendo moja hai kipeo la Upendo wa Utatu, cheche hai hii ilipochemka, malaika walishangilia, kwa sababu nuru hai zaidi ilikuwa haijaonekana Mbinguni. Kama petali ya waridi la Mbinguni juu, petali isiyo na mwili, kito cha thamani na mwako, iliyokuwa pumzi ya Mungu ishukayo iuhishe ule mwili namna mbali sana na nyingine. Cheche hiyo ilishuka kwa nguvu jinsi hii katika moto wake hata Kosa halikuweza kuiharibu, ikapita anga na kujifunga ndani ya tumbo takatifu.

Dunia ilikuwa na Ua lake, ijapo haijapata kujua. Ua la kweli na la pekee lachanualo milele: yungiyungi na waridi, mwalizeti na yasmini, na maua mengine ya manukato, yote yameungana pamoja, nayo maua yote ya dunia kuwa Ua moja, Maria, ambaye anajumlisha ndani yake fadhili ya kila aina pamoja na neema zote.

Mwezi wa Aprili nchi ya Palestina ilionekana bustani kubwa ajabu, na harufu nzuri na rangi yote yalifurahisha mioyo ya watu. Lakini Waridi nzuri kuliko zote haijajulikana bado. Yeye alianza kusitawi kwa Mungu faraghani ndani ya tumbo la mama, kwa kuwa

15

Mama yangu alipenda tangu kutungwa kwake. Lakini mzabibu unapotoa damu yake kwa kufanya divai tu, na harufu ya maji ya zabibu, yenye sukari na kali, inapojaza viwanja na pua, Yeye atatabasamu mbele za Mungu kwanza na mbele ya watu baadaye, akisema kwa kicheko chake safi kabisa: “Tazameni, mzabibu utakaowapeni kichala cha kushindiliwa shinikizoni ili igeuke dawa ya

uzima kwa maradhi, mzabibu huu ni kati yenu".

Nalisema "Maria alipenda tangu kutungwa kwake". Ni kitu gani kinachoipa roho mwanga wa ujuzi? Neema. Ni nini inayoondoa Neema? Dhambi ya asili na dhambi ya mauti. Maria, Asiye na Mawaa, hakuishiwa na ukumbuko wa Mungu, na ushirika wake, na upendo wake, na nuru yake, na hekima yake. Yeye kwa hiyo aliweza kujua na kupenda alipokuwa na mwili tu uliogandama kuzunguka roho isiyo na dhambi iliyoendelea kupenda.

4.7 7 Obele zaidi nitakutazamisha kwa moyo ukina wa ubikira wa Maria. Utapatwa na kizunguzungu cha mbinguni kama wakati nilipokuonyesha umilele wetu. Sasa ufikiri kama mama akikichukua mimba kiumbe bila kosa, ambalo lingetenga na Mungu, ingawa mimba alipata kwa njia ya kibinadamu, kawaida, apewe akili ya juu na kuwa nabii. Nabii wa binti yake, ambaye yeye anamwita: "Binti Mungu". Na ufikiri jinsi ingalikuwa kama kutoka Wazazi wa kwanza bila hatia wangelizaliwa wana bila hatia, kama Mungu alivyo panga.

Enyi watu mnaosema kuelekea "mtu mkubwa" na kwa upotovu wetu mnaelekea ibilisi mkubwa tu!" Hiyo ndiyo ingalikuwa njia ya kuelekea 'mtu mkubwa': kuweza kukaa pasipo upotovu wa Shetani kwa kumwachia Mungu utawala wa maisha, wa ujuzi, wa wema, msipotamani zaidi ya kiasi - na ilikuwa kidogo punde tu kuliko yote - Mungu angaliwapa kwa kuweza kuzaa, katika mageuzi yenye kuendelea kwa ukamilifu, wana ambao wangukuwa watu mwilini na wana wa ufahamu rohoni, yaani washindaji, yaani wahodari, yaani Madubwana dhidi ya Shetani. Shetani huyo na pamoja naye uovu wake wote angaliangushwa tangu zamani badala ya wakati itakapowadia".

5 , Kuzaliwa kwa Maria.

Ubikira wake katika fikira ya milele ya Baba.

26 Agosti 1944.

5.1 1 Ninaona Ana anayetoka bustani. Anamtegemea mkono wa mwanamke wajamaa kweli, kwa sababu anamfanana. Ni mzito sana na

16

yaonekana amechoka huenda pia kwa hari, iliyo kama ile inayonilegeza sasa.

Ingawa bustani ni penye kivuli, hata hivyo hewa ni nzito, yenye moto. Hewa ya kukatwa kama kinyunya kitefufu na cha moto, hata ni nzito, chini ya uwingu wa kibuluu hata uvumbi ulioko unaigeuza kuwa nyeusi kidogo. Tangu zamani imepaswa kuwa kavu, va sababu ardhi pasipomwagiliwa maji, imegeuza kuwa tifufu na karibu nyeupe. Pengine rangi yake ielekayo nyekundu chafu, na ngi ya ngeu ikiwa majimaji, chini ya miti au kandokando ya ngwe ndogo panapoota mistari ya mboga, na kuzunguka miwaridi na yasamini, na maua mengine yaliyo hata mbele na kandokando ya matao mazuri yatengayo bustani nusu kwa nusu mpaka mwanzo wa mashamba zilikokwisha ondolewa nafaka. Na nyasi za shamba pia, laonyeshalo mwisho wa hozi, ni kavu na chache. Kandokando yake tu, palipo ua wa miti wenye maua madogo mengi rangi ya yakuti, nyasi ni rangi majani na nzito, na pale, wakitafuta malisho na kivuli wapatikana kondoo wachache na mtoto mmoja mchungaji.

